SportPesa
TZS. 1,042,431,860
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Anusurika** kifungo maisha jela kesi dawa za kulevya

UKURASA 4



**USHINDI MFULULIZO KICHEKO KWA KLOPP**

UKURASA 21

Nipashe
Ijumaa Machi 18, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580888
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Samia awatoa hofu wananchi wa Chato

• **Kuhusu** miradi iliyoanzishwa na JPM, ibada kumbukizi yafanyika, Mwinyi, wadau waeleza atakavyokumbukwa... *Endelea ukurasa 2 & 4*



Rais Samia Suluhu Hassan, akimfariji Mama Janeth Magufuli, baada ya kuweka shada la maua katika kaburi la aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Pombe Magufuli, wakati wa Misa Takatifu ya kumbukizi ya mwaka mmoja tangu afariki, Uwanja wa Michezo wa Magufuli, wilayani Chato mkoani Geita jana. **Picha ndogo:** Rais Samia, akisaini kitabu cha kumbukumbu kabla ya kuweka shada la maua. **PICHA: IKULU**




## Sangoma asakwa kwa madai kumpa ujauzito mwanafunzi

UKURASA 3

## Mbaroni tuhuma kusambaza video ya mgonjwa Muhimbili

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA KUMALIZA MAKUNDI KIBABE UK.24
MAONI, KATUNI UK.6




Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu (wapili kushoto), akikabidhi moja kati ya kompyuta mpakato tano kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, zilizotolewa na benki hiyo, kwa ajili ya Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA), jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Katibu wa Machinga Kariakoo, Thabit Maloka na Meneja Uhusiano Biashara za Serikali wa benki hiyo, Mkunde Joseph. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia awaondoa hofu Chato

**Na Lilian Lundo,** MAELEZO

RAIS Samia Suluhu Hassan amewatoa hofu wananchi wa Chato kwamba miradi yote iliyopangwa na iliyoanza kutekelezwa wilayani hapo itakamilika kama ilivyopangwa.

Miradi hiyo ni ile iliyoanzishwa na serikali ya awamu ya tano chini ya Hayati Rais John Magufuli kama vile uwanja wa ndege, stendi ya mabasi hospitali ya rufani ya kanda na uwanja wa michezo.

Samia aliyasema hayo jana mjini hapo wakati wa kumbukizi ya mwaka mmoja wa kifo cha Hayati Magufuli iliyofanyika uwanja wa michezo Chato iliyoambatana na ibada maalum iliyoongozwa na Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Geita, Flavian Kasala.

"Kwa hapa Chato nataka niwahakikishie kwamba miradi yote tuliyopanga na ambayo tumeshaanza kutekeleza, tutaikamilisha hata ile midogo midogo," alisema Rais Samia huku akisisitiza kuwa itakapokamilika atakwenda kuifungua.

Alisema anafahamu juu ya ujenzi wa kivuko cha Hapa Kazi Tu kinachofanya kazi kati ya Chato na Nkome ambacho kimekamilika kwa asilimia 100 na kimegharimu Sh. bilioni 3.1.

Miradi mingine ni ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Chato ambao umefikia asilimia 95 kwa gharama ya Sh. bilioni bilioni 58.9 na stendi mpya ya Chato ambayo imegharimu Sh. bilioni 13.2 na ujenzi wake umefikia asilimia 90 na mabasi madogo yameshaanza kuingia.

Pia alisema amearifiwa kuwa ujenzi wa hospitali ya rufani ya kanda inayojengwa kwa Sh. bilioni 34 unaendelea vizuri na baadhi ya huduma zimeanza kutolewa.

"Nataka niwaahidi Wanachato, miradi hii itakapokamilika kabisa, nitakuja mwenyewe kuifungua kama ambavyo angefanya Dk. Magufuli kama angekuwapo," alisisitiza Rais Samia.

Pia alisema serikali imeendelea kuboresha na kuendeleza huduma za jamii zikiwamo afya, maji, elimu na umeme kama inavyoelekezwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kama walivyojipanga kutekeleza.

"Mtakumbuka katika hotuba yangu ya mwanzo kabisa baada ya kuapishwa nilisisitiza kwamba nitayaendeleza mema yote aliyotuachia Hayati Magufuli na kuleta mema mengine mapya," alisema.

Pia alisema wanataka kujenga Tanzania ya kisasa na kuboresha maisha ya Watanzania wote na hayo yote yatafanikiwa ikiwa, umoja, amani na mshikamano miongoni mwa Watanzania vitadumishwa.

Katika hatua nyingine, Rais Samia aliwashukuru viongozi wa dini kwa kuendelea kuliombea taifa na kuliweka mikononi mwa Mwenyezi Mungu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe:@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**DODOMA,**
**17 - 03 - 2022**

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 23-03-2022 hadi 26-03-2022 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea JNHPP SITE, gari hilo lenye namba za usajili: **T 836 DSC / T 777 AQR**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 18.5**
   **Upana - mita 7.20**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi JNHPP SITE kupitia KILWA ROAD, KIBITI, MLOKA.** Gari litasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka **Dar es Salaam Port mpaka Bungu.** Kutoka **Bungu kwenda JNHPP** Site gari litasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

216757302

## Mradi umeme Nyerere waleta matumaini

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Nishati, January Makamba, amesema utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) umefikia asilimia 56.

Mradi huo utakapokamilika utazalisha umeme wa megawati 2,115.

Makamba aliyasema hayo juzi Rufiji mkoani Pwani wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyolenga kukagua utekelezaji wa mradi huo.

Alisema mradi wa JNHPP kwa sasa unatekelezwa kwa kasi kutokana na maboresho mbalimbali yaliyofanyika katika usimamizi na uendeshaji wa mradi huo. Makamba alitaja baadhi ya maboresho hayo ni kuongeza utaalam na wataalam, kwamba mkandarasi anayetekeleza mradi huo, Kampuni ya Elsewedy Electric amehimizwa kuongeza wataalam wenye uzoefu wa usimamizi.

Alitaja maboresho mengine kuwa ni mabadiliko ya uongozi katika mradi, kubadili mfumo wa mawasiliano kati ya Wizara na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

# JPM akumbukwa kwa ibada maalum

**Na Richard Makore,** CHATO

HUZUNI na simanzi vilitawala jana katika misa maalumu ya kumbukizi ya mwaka mmoja tangu kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, wilayani Chato, mkoani Geita.

Misa hiyo maalumu iliongozwa na Askofu wa Jimbo Katoliki la Geita, Flavian Kasala.

Wananchi walionekana wakiwa na nyuso za huzuni na simanzi huku baadhi yao wakilia kimya kimya na kufuta machozi.

Wananchi hao walianza kuingia uwanja wa Magufuli nje kidogo ya mji wa Chato saa 12 asubuhi.

Wakati mahubiri yakiendelea, wananchi walionekana kutulia wakitafakari huku wengine wakitokwa machozi.

Katika mahubiri yake, Askofu Kasala alitaka watu kutenda haki kwa wenzao bila kujibakiza.

Aliwauliza wananchi waliofika uwanjani hapo kama mtu akifa leo ataingia mbinguni?

Alisema watu wakipata majibu ya swali hilo, watambue hayati Magufuli anahitaji huruma na msamaha wa Mungu.

Alisema katika ubinadamu ni ngumu ukawa mpole mpaka kumridhisha Mungu, inawezekana ikawa ngumu.

"Watu watende haki kwa watu wote bila kujibakiza katika maisha yao hapa duniani," alisema Askofu Kasala. Kadhalika, alisema ili mtu asimamie haki mpaka akaudhi wenzake ni lazima kujitoa sadaka na kipimo hicho ndicho kinachowapa walio hai nguvu za kuwaombea marehemu.

Askofu Kasala alisema mema ya marehemu Magufuli yawe dira kwa maisha ya waliobaki duniani.

Alisema wamekusanyika jana wakiwa wanamwombea marehemu Magufuli apate huruma za Mungu na sio vinginevyo.

"Magufuli aliishi katika ubinadamu, amekuwa kiongozi ametuongoza, katika uongozi wake huo hakuna hata heri moja tuliyoona?" Alihoji Askofu Kasala. Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamure, akizungumza katika kumbukizi hiyo, alisema kwa sasa hawafanyi tukio hilo wakiwa na huzuni kwa kuwa wanaye mtu anayewafariji.

Alisema Rais Samia ameendelea kuwashika mkono wananchi wa Geita pamoja na Wilaya ya Chato kwa kuwapa fedha nyingi za miradi ya maendeleo.

Pia amekuwa mfariji wao tangu kifo cha hayati Magufuli hadi sasa jambo ambalo linawaondolea huzuni.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Ibrahim Juma, alisema hayati Magufuli alisaidia mhimili huo kuhamia Dodoma. Alisema hayati Magufuli hakupata muda wa kutosha kuandika historia ya maisha yake hapa duniani.

Rais Samia Suluhu Hassan aliingia uwanjani hapo saa 10.02 asubuhi na kuongoza wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi katika kumbukizi hiyo.

Akizungumza katika kumbukizi hiyo, Rais Samia aliahidi kujenga Tanzania ya kisasa na kuwa miradi yote iliyoanzishwa na hayati Magufuli itakamilika.

Aliwaomba Watanzania kushiriki uwekaji wa anwani za makazi katika maeneo mbalimbali hapa nchini huku akitoa wito mwaka huu kuhesabiwa.

Aliitaka jamii kufichua watu wenye ulemavu ili wahesabiwe huku akiwaomba viongozi wa dini kusaidia jambo hilo.

Akitoa salamu kwa niaba ya familia, mjane wa hayati Magufuli, Janeth Magufuli, alisema siku ya jana ilikuwa ni maalum kwa ajili ya kumwombea mpendwa wao.

Alisimulia namna alivyompigia simu Rais Samia kumualika kushiriki misa hiyo na ombi lake lilikubaliwa. Kumbukizi hiyo iliambatana na mvua kubwa iliyonyesha katika maeneo mbalimbali wilayani Chato ikiwamo katika viwanja vilivyofanyika kumbukizi hiyo.

Hayati Magufuli alifariki dunia Machi 17, mwaka jana, jijini Dar es Salaam na kuzikwa nyumbani kwake wilayani Chato, mkoani Geita.

## HABARI KITAIFA

# Mfalme Zumaridi aingia kortini kwa staili mpya

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MUNGU chini ya jua, Mchungaji Diana Bundala maarufu Mfalme Zumaridi, jana alingia katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya mkoani Mwanza na staili mpya ya kujifunika uso.

Mfalme huyo anayekabiliwa na mashtaka matatu ambayo ni kufanya kusanyiko lisilokuwa halali, kuzuia maofisa wa serikali kutekeleza majukumu yao na usafirishaji haramu wa binadamu, jana alifikishwa mahakamani hapo pamoja na wafuasi wake majira ya asubuhi na kupandishwa kizimbani majira ya mchana, huku ulinzi ukiimarishwa ipasavyo na askari wa Jeshi la Polisi nje ya majengo ya mahakama ya hakimu mkazi ikiwa ni tarehe ya kutajwa kwa kesi yao.

Mfalme huyo ambaye ana wafuasi wengi katika kanisa lake jijini Mwanza, alionekana mahakamani hapo mwenye huzuni na sura iliyokosa matumaini ambapo washtakiwa wote walisomewa mashtaka yao na mawakili wa serikali, Dorcas Akyoo na Merito Ukongoji mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, Monica Ndyekubora.

Baada ya washtakiwa hao kufikishwa mahakamani hapo ili kusomewa maelezo ya awali ya makosa yanayowakabili, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Dorcas Akyoo, aliomba mahakama kuahirisha kusikiliza maelezo ya awali kwa madai kuwa upande wa Jamhuri kutokamilisha upelelezi na mahojiano ya mashtaka ya makosa yanayomkabili Diana Bundala na wenzake katika mashtaka yote yanayowakabili.

Hivyo wakili huyo wa serikali akaiomba mahakama kuruhusu kusomewa mashtaka kwa washtakiwa wawili katika shauri namba 10 linalomkabili Diana Bundara la kumshambulia na kumjeruhi askari wa Jeshi la Polisi mwenye namba PF19154 Mkaguzi wa Polisi James Mgaya kosa wanalodaiwa kulifanya washtakiwa hao kinyume na kifungu namba 241(46)cha sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 46 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Pia katika kosa la pili washtakiwa hao wanashtakiwa kwa kosa la kumzuia ofisa wa polisi kutekeleza majukumu yake kosa wanalodaiwa kulitenda tarehe 23/2/2022 kwa askari huyo kutekeleza amri ya Mahakama ya Mwanzo Mkuyuni kinyume na kifungu cha 243 b cha kanuni ya adhabu sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Katika shtaka la tatu washtakiwa hao wanashtakiwa kwa kosa la kumzuia ofisa wa umma kutimiza majukumu yake kinyume na kifungu cha 114a(b) cha sheria ya kanuni ya adhabu iliyofanyiwa marekebisho 2019 washtakiwa wote walikana mashtaka yanayowakabili.

Katika hatua nyingine wakili wa utetezi, Erick Muta, aliiomba mahakama kuruhusu washtakiwa wengine 34 kupewa dhamana ombi ambalo lilikubaliwa na Hakimu Ndyekubora na kuagiza taratibu zote kufuatwa ikiwamo kufika mahakamani hapo kila shauri linapotajwa.

Hata hivyo, wakili huyo amelalamikia hatua ya wateja wake kutopewa chakula wakati wakiwa mahakamani, na akaiomba mahakama kutoa amri ya kuruhusu kupewa chakula ombi, ambalo Ndyekubora alilitolea ufafanuzi kwa kueleza kuwa utaratibu wa chakula kwa mahabusu uko chini ya Jeshi la Magereza kwa mujibu wa sheria na taratibu.

# Mbaroni tuhuma kusambaza video ya mgonjwa Muhimbili

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) limemshikilia Allen Mhina (31) mkazi wa Temeke Mwembeyanga na wenzake 13 kwa tuhuma za kusambaza video katika mitandao ya kijamii kinyume na sheria.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa Allen ambaye ni Mkurugenzi wa mtandao wa kijamii wa U-turn Collection na wenzake, walihusishwa na kusambaza video ikimwonyesha mmoja wa wagonjwa aliyekuwa amelazwa kwenye chumba cha uangalizi maalum (ICU) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Alisema suala la kusambaza video hizo lilileta taharuki kwa hospitali hiyo na wafanyakazi wake huku akibainisha kuwa watuhumiwa hao walikutwa na vifaa mbalimbali vya kielektroniki vya kiuchunguzi vikiwamo kamera, kalamu, saa, funguo, miwani, kofia, kompyuta mpakato (laptop) na 'memory card' ambavyo vyote vinachunguzwa.

"Kitendo kinachotuhumiwa kufanywa na watuhumiwa hao kililenga kudhalilisha, kutia hofu au kuleta taharuki suala ambalo linalazimisha mamlaka hizi mbili za kisheria kuchunguza kwa kina jambo hilo. Uchunguzi unaendelea na pindi ukikamilika watafikishwa kwenye vyombo vingine vya kisheria," alisema Muliro.

Pia alisema Januari na Februari, mwaka huu, jeshi hilo liliwakamata watu wengine 11 kwa tuhuma za utapeli wa viwanja na kujipatia Sh. milioni 100 kwa njia ya udanganyifu, wakijifanya wanamiliki na kuuza viwanja vya makazi ambavyo si vyao.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa Goba, Dar es Salaam baada ya kuwatapeli masista wa Kanisa Katoliki Shirika la Mabinti wa Mtakatifu Maria Kipalapala. Alisema watuhumiwa hao watafikishwa kwenye vyombo vingine vya kisheria kwa hatua zaidi.

Pia alisema kuwa jeshi hilo bado linaendelea na operesheni kali dhidi ya vikundi mbalimbali vinavyojihusisha na uhalifu vikiwamo wizi wa pikipiki, bajaji na magari.

"Pia jeshi limefanikiwa kuwakamata watuhumiwa 41 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam wakiwa na pikipiki 29 za wizi na zingine zinazotumika kufanyia uhalifu.

Jeshi linawaomba wananchi waendelee kutoa taarifa mbalimbali ili zifanyiwe kazi ili vitendo vya kihalifu viweze kupungua," alisema Muliro.




Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Suzanne Ndoma, akizungumza katika uzinduzi wa awamu ya nane ya programu ya mafunzo kwa wanawake viongozi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sangoma asakwa madai ya kumpa ujauzito mwanafunzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MGANGA wa kienyeji mkoani hapo, Juma Kipanya anatafutwa na polisi kwa tuhuma za kumpa ujauzito mwanafunzi wa shule ya msingi na kukatisha ndoto ya kuendelea na masomo.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani hapo, Foka Dinya, akizungumza na mwandishi wa habari ofisini kwake, alisema wanaendelea kumtafuta mtuhumiwa huyo ili afikishwe mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili, likiwamo la kumkatisha masomo mwanafunzi huyo.

Mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 15 alikuwa anaingia darasa la saba na inadaiwa kupewa ujauzito na mganga huyo mwishoni mwa mwaka 2021, baada ya kuitwa na mganga huyo kusaidia kutengeneza dawa za kutibu ugonjwa uliokuwa unamsumbua babu yake.

Kaimu Kamanda Dinya akizungumzia taarifa za mganga huyo, alisema wanaendelea kumtafuta mtuhumiwa huyo ili afikishwe kwenye vyombo vya sheria kujibu mashtaka yanayomkabili, likiwamo la kubaka, kumpa ujauzito na kukatisha ndoto za mwanafunzi huyo.

Alisema mtuhumiwa alitoroka baada ya kupata taarifa ya kutafutwa kujibu mashtaka yanayomkabili.

Kamanda Dinya alisema mwanafunzi huyo akiwa nyumbani kwa mtaalamu huyo kutekeleza majukumu aliyopewa, mganga alianza kumtaka kimapenzi mwanafunzi huyo na alipomkatalia, alimpa vitisho kuwa atamwadhibu.

"Mwanafunzi huyu kwa sasa ana ujauzito wa miezi saba, na yupo nyumbani chini ya uangalizi wa mama yake mzazi akisubiri kujifungua," alisema Kamanda Dinya.

Akizungumza na mwandishi habari hizi nyumbani kwao, mwanafunzi huyo alisema, yeye na mama yake walikataa kwenda kwa mganga huyo kwa kile walichodai amekuwa na tabia chafu ya kuwataka kimapenzi wateja wanawake wanaofika kupewa tiba.

Naye mama mzazi wa mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa), alisema mwezi Juni mwaka jana alipokea simu kutoka kwa mkwewe, akimtaka mtoto huyo kwenda kwa mganga kumfanyia dawa babu yake, lakini alimkatalia kutokana na tabia chafu aliyonayo mganga huyo.

"Siku moja tukiwa nyumbani hapa nikapigiwa simu na babu yake akimtaka mtoto kwenda kwa mganga akamtengezee dawa, lakini kwa vile tabia ya mganga yule inafahamika nilikataa asiende," alisema mama huyo.

Hata hivyo, alisema kaka zake wawili walifika nyumbani wakiwa na pikipiki na kumlazimisha mtoto aende kwa mganga huyo na asipokubali watamwadhibu kwa kumpa kipigo, hali iliyomlazimu mama amruhusu na kuondoka kwa shin-

HABARI KITAIFA

# Rais Mwinyi ataja alama za kumkumbuka Magufuli

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Watanzania wataendelea kumkumbuka na kumuenzi Hayati Dk. John Magufuli kwa kuendeleza falsafa na maono yake pamoja na mambo mazuri aliyoyafanya kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika uwanja wa Magufuli, Chato mkoani Geita, wakati akitoa hotuba yake katika kumbukizi ya mwaka mmoja wa kifo cha Hayati Dk. Magufuli, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Tanzania. Tukio hilo la kumbukizi liliongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan ambalo liliambatana na Ibada ya Misa Takatifu iliyoongozwa na Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Geita, Flavian Kasala.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, Watanzania wataendelea kukumbuka uongozi wa Hayati Dk. Magufuli uliokuwa umetawaliwa na busara, umahiri na ujasiri.

Katika hotuba yake hiyo, Rais Dk. Mwinyi aliwafikishia wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki, wananchi wa Chato na Watanzania wote salamu za upendo kutoka kwa wananchi wa Zanzibar.

Alisema kutokana na alama alizoziacha Magufuli kwa maendeleo ya taifa pamoja na namna kifo chake kilivyogusa na kusononesha nyoyo za Watanzania, inaonekana kama vile kimetokea wiki chache zilizopita na si mwaka mmoja uliopita kama ilivyo katika uhalisia.

Kwa mujibu wa Rais Mwinyi, Watanzania wataikumbuka kwa majonzi makubwa Machi 17, mwaka jana, walipopokea kwa mshtuko taarifa ya kifo chake na majonzi makubwa wakati wa mazishi yake Machi 26, mwaka jana.

"Tutaendelea kujifunza kutokana na historia yake kwa kutumia nadharia mbalimbali alizotuachia katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na ustawi wa jamii," alisema.

Dk. Mwinyi alisema wakati Magufuli anakumbukwa na kuenziwa na kumwombea dua, Watanzania wanamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwapa mrithi madhubuti, shupavu, mwenye nia thabiti, uoni na ujasiri wa kuendeleza mambo mazuri aliyoyaacha marehemu pamoja na viongozi wengine wa taifa wa awamu zilizotangulia katika pande zote za Muungano.

Alisema kauli mbiu aliyokuja nayo Rais Samia baada ya kurithi kiti cha marehemu inayosititiza kwamba 'Kazi Iendelee' ni ushahidi wa dhamira yake ya kuendeleza mambo mazuri yaliyoachwa na Magufuli pamoja na viongozi walioongoza kabla yake.

Rais Dk. Mwinyi alisema ni jukumu la Watanzania wote kuendeleza kazi hiyo kwa kadri ya uwezo wa kila mtu na ni wazi kuwa kaulimbiu hiyo ni njia bora ya kumuenzi Hayati Dk. Magufuli ambaye ametimiza mwaka mmoja tangu kifo chake.

Alisema njia bora kwa Watanzania ni kuendelea kuchapa kazi kwa kuzingatia misingi ya uwajibikaji, uzalendo na uadilifu.

Alisisitiza kwamba kazi iendelee kwa kuendeleza yote mazuri yaliyofanywa na marehemu katika masuala muhimu na mazito yanayohusu maendeleo na kuendelea kuhakikisha kuwa kunakuwa na matumizi bora na endelevu ya rasilimali zilizoko.



Wajumbe wa Bodi ya DAWASA wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange (wapili kulia), wakipata maelezo ya uendeshaji wa mtambo wa kuzalisha maji wa Ruvu Juu kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja (watano kulia), walipofanya ziara kutembelea miradi ya majisafi inayosimamiwa na kutekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam na Pwani, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Anusurika kifungo cha maisha jela

Na Kulwa Mzee

MFANYABIASHARA Remina Abdul, amenusurika kutumikia kifungo cha maisha jela kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya baada ya Mahakama ya Rufani Tanzania kukubali hoja za kupinga adhabu na kwamba hakukuwa na ushahidi wa kutosha kumtia hatiani na kumpa adhabu hiyo.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mbele ya jopo la majaji watatu, Shaaban Lila, Jaji Lugano Mwandambo na Jaji Lilian Mashaka, baada ya kupitia sababu za kupinga hukumu ya Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Katika hati ya mashtaka ilidaiwa kuwa Remina, mwanawe, Maemba Jonathan na kaka yake Saidi Kitalo, walikamatwa maeneo ya Kinondoni, Mtaa wa Ufipa Agosti 29 mwaka 2017, wakituhumiwa kufanya biashara ya kusafirisha dawa za kulevya.

Washtakiwa wanadaiwa kukutwa na dawa hizo aina ya heroine hydrochloride gramu 201.38.

Kesi hiyo ilisikilizwa na Jaji Elinaza Luvanda, washtakiwa wengine waliachiwa mwaka 2020 na mrufani akatiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo cha maisha jela.

Upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi wanane na vielelezo vya nyaraka halisi ambavyo walitoa mahakamani. Inadaiwa msiri alitoa taarifa kwa SSP Salmini kuwa kuna washukiwa wa biashara ya dawa za kulevya maeneo ya Kinondoni, mtaa wa Ufipa.

Askari sita walikwenda katika nyumba ya Remina, washtakiwa walikuwa nje ya nyumba kwenye baa, lakini hakukuwa na wateja.

Upekuzi ulifanyika katika chumba cha kulala na sebuleni ambako dawa hizo zinadaiwa kukutwa.

Mlalamikaji Remina alidai ni mfanyabiashara wa duka, anapika chakula na saluni na alikamatwa usiku na polisi waliokuwa na silaha.

Alidai kuwa baada ya kujitambulisha alipigwa na kupelekwa katika gari la polisi pamoja na watuhumiwa wengine na kufikishwa Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam ambako walilala hadi siku iliyofuata walipopelekwa maeneo ya Upanga, ambako alidai kuwa aliteswa ili akiri.

Mrufani alidai kulazimishwa kusema kwamba mwanawe Maemba anajihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Alidai kuwa alipokiri alipigwa picha na baadaye walirudishwa polisi kisha kufikishwa mahakamani Oktoba 12, 2017.

Mrufani akiwakilishwa na Wakili Nehemiah Nkoko, alitoa sababu kadhaa za kupinga adhabu ikiwamo Jaji alijielekeza vibaya katika kupokea vielelezo ambavyo havikutajwa katika orodha ya vielelezo wakati Jamhuri wanasoma maelezo ya mashahidi katika mahakama ya chini.

Ilidaiwa jaji alishindwa kuchambua vizuri ushahidi wa Jamhuri kabla ya kutoa uamuzi kwamba Jamhuri wamethibisha makosa dhidi ya mrufani bila kuacha shaka.

Wakili Nehemia alidai hati ya mashtaka haikuwawezesha wahusika kujitetea na hoja nyingine, mrufani hakutendewa haki kutiwa hatiani na kupewa adhabu hiyo. Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Waziri Magumbo ambaye alipingana na hoja za upande wa mashtaka, akisisitiza kwamba makosa dhidi ya mrufani yalikuwa yamethibitika bila kuacha shaka.

Jopo hilo lililoongozwa na Jaji Lila katika uamuzi wake lilisema hakuna ushahidi wa kutosha kumtia hatiani na kumpa adhabu ya kifungo cha maisha mrufani.

"Mahakama imekubali rufani, hatia na adhabu dhidi ya mrufani vinaondolewa na Mahakama inaamuru mrufani aachiwe huru."

## Dar wamkumbuka JPM mapambano dhidi ya UVIKO-19

Na Jenifer Gilla

KATIKA kuadhimisha mwaka mmoja tangu Rais wa Awamu ya Tano, Dk. Joseph Magufuli afariki dunia, baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wamesema watamkumbuka kwa ujasiri wake katika kupambana na UVIKO-19.

Rhoda Nyambuya (35), mkazi wa Boko, jijini Dar es Salaam, alisema kuwa ujasiri wa hayati Magufuli wakati ugonjwa huo unaingia nchini kwa mara ya kwanza umechangia watu kuondoa hofu, kuudhibiti na kuwafikia walipo.

"Ugonjwa huu ulipotangazwa kuingia nchini kwa mara ya kwanza Machi, 2020, Watanzania tulipata uoga kutokana na tulivyoshuhudia mataifa yaliyotangulia kuupata kama vile China, Italia watu wake walivyokuwa wanakufa, lakini alitufundisha kuwa tukiuogopa ugonjwa huo ndiyo utatumaliza hivyo tuchukue tahadhari huku tukimwamini Mungu," alisema Rhoda.

Alisema ujasiri huo pamoja na utamaduni wa kufuata maagizo ya kujikinga na ugonjwa huo kutoka Wizara ya Afya, ikiwamo kuvaa barakoa, kuepuka mikusanyiko isio ya lazima vilisaidia kwa kiasi kikubwa kuudhibiti ugonjwa huo.

"Katika kukabili janga lolote la kitaifa Rais anapoonyesha uoga mwanzoni basi ujue hata wananchi watakuwa hivyo hivyo, tunamshukuru Magufuli alivaa ujasiri na kutuaminisha kuwa tukiamua ugonjwa huu tunaweza kuudhibiti mapema na ndivyo ilivyokuwa," alisema.

Naye Doris Peter (43), fundi cherehani wa Ubungo, alisema anamkumbuka Hayati Magufuli kwa kuwaonyesha fursa ya kibiashara iliyoletwa na janga la UVIKO-19.

"Kupitia mafunzo ya Rais nilijifunza kutengeneza barakoa za kushona na kuwauzia watu kwa Sh. 2,000 hali iliyoongeza kipato changu, biashara ambayo mpaka sasa naifanya ingawa mauzo sio makubwa kama hapo mwanzo," alisema Doris.

Akizungumzia mafanikio yaliyoletwa na biashara ya barakoa, Doris alisema alikuwa akiuza kila barakoa kwa Sh. 1000 na kuwa na uhakika wa kupata Sh. 5,000 kwa siku.

Naye Peter Mmari (50), mkazi wa Tabata, Dar es Salaam alisema, anamshukuru Rais kwa kuwaruhusu Watanzania watumie njia za asili katika kupambana na ugonjwa huo kwa kuwa ilisaidia kupunguza kasi ya maambukizi.

"Ule mpango wa kutumia dawa za asili za kujifukiza, ulisaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo kwa sababu watu walikuwa wanajihudumia wenyewe pale wanapohisi wamepata maambukizi," alisema na kuongeza:

"Nakumbuka mtaani kwetu baadhi ya shughuli za kijamii kama misiba ilikuwa sio rahisi kukwepa kushiriki, basi mtu akitoka pale msibani anakata mti wa mwarobaini anajifukiza usiku na asubuhi maisha yanaendelea, hii ilisaidia sana kupunguza kuenea kwa ugonjwa huu maana tungekufa wengi sana."

Naye Richard Philemon, mfanyabiashara wa nguo Kariakoo, alisema kuwa kitendo cha rais kutofunga shughuli za kibiashara na kazi licha kuwapo wa ugonjwa huu ni cha kishujaa kwa kuwa kimewasaidia Watanzania na nchi kwa ujumla kutoathirika sana kiuchumi.

HABARI PICHANI

# KUMBUKIZI YA MWAKA MMOJA WA HAYATI DK. JOHN MAGUFULI




Wananchi mbalimbali wakiwa katika ibada ya kumbukizi ya mwaka mmoja wa Hayati Dk. John Magufuli, iliyofanyika jana katika Uwanja wa Michezo wa Chato, mkoani Geita.






Rais Samia Suluhu Hassan akiweka shada la maua katika kaburi la Hayati Dk. Magufuli. Picha kulia ni Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiweka shada la maua.

**PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwasili mjini Chato kwa ajili ya kushiriki kumbukizi ya mwaka mmoja ya Hayati Dk. Magufuli.



Rais Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na mjane wa Hayati Magufuli, Mama Janet.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wito wa Samia mmomonyoko wa maadili uzingatiwe

**CHANZO** cha vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyoendelea kushamiri kwa wanawake na watoto nchini, kinatajwa kuwa ni kasi ya mmomonyoko wa maadili katika jamii, ambapo wazazi na walezi wanatakiwa kupaza sauti na kuvifichua.

Rais Samia Suluhu Hassan aliyabainisha hayo wakati akizungumza na watu wenye ulemavu Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma, huku akionyesha kukerwa na jinsi ambavyo jamii inavyozidi kuharibika.

Kwa mujibu wa Rais, tatizo linaanzia ndani ya familia, na anawataka wazazi watimize wajibu wao wa kusimamia maadili mema ili tatizo hilo likifika ngazi ya taifa liwe limeshafanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa.

Sisi tunaungana na Rais kwa kukemea hadharani mmomonyoko wa maadili katika jamii, ili kujenga taifa la watu wanaheshimiana na kuzingatia maadili mema ni chanzo cha kuepuka vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Tunatambua kuwa maadili yanasaidia kumwelekeza mtu katika njia sahihi ambayo humwezesha kutenda matendo mema katika jamii inayomzunguka, hivyo kumjengea uaminifu na kuepuka migongano.

Kimsingi, maadili mema kwenye jamii tunatambua kuwa ni msingi mzuri ambao kwa namna moja au nyingine humfanya mtu kuwa mwema, hivyo ni vyema kila mmoja aungane na Rais kukemea mmomonyoko wa maadili.

Tujuavyo ni kwamba, suala la malezi mema kwa watoto ni jukumu la kwanza la wazazi, ambalo hawanabudi kulitimiza kwa kushirikiana na jamii na tena kwa ustahimilivu mkubwa.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, watoto wanapitia hatua mbalimbali za ukuaji hadi ujana ambao ni kipindi cha mabadiliko ya haraka katika mfumo mzima wa maisha, hivyo tunaona suala la malezi ni la muhimu.

Kwa maana hiyo, tunakubaliana na Rais kuhamasisha jamii kuwa makini katika malezi, kwani siyo siri kuwa watu wanaishi katika mchanganyiko wakiwamo wasiojali hali ambayo inaweza kusababisha mmomonyoko wa maadili.

Hatua ya Rais kutaja chanzo cha ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, ni wazi ipo haja kwa jamii kurejea kwenye malezi ambayo yanazingatia maadili mema ili vitendo au viashiria vya mmomonyoko wa maadili visiwepo nchini.

Kwa kauli hiyo ya Rais, tunadhani ungekuwa ni wakati sahihi kwa Watanzania kila mmoja kwa nafasi kukaa na kutafakari ni wapi amekosea katika malezi ili kusaidia kupunguza kama siyo kumaliza kabisa ukatili huo katika jamii.

Iwapo wazazi na walezi watakaa kimya bila kusimamia malezi mema, tunaona kuwa watakuwa wanachangia kwa kiasi kikubwa mmomonyoko wa madili kwa watoto wao, hivyo ushauri wetu ni kwamba jamii ibadilike.

Labda tuwakumhushe kuwa katika dunia ya leo kumekuwapo na mabadiliko mengi katika nyanja za mbalimbali kuanzia elimu, afya, uchumi, mawasiliano, hali ambayo wazazi wanakuwa mbali na watoto.

Katika mazingira hayo, watoto wanaweza kujifunza tabia ambazo zinakwenda kinyume na maadili mema, hali ambayo ni rahisi kujiingiza kwenye vitendo visivyofaa vilivyosababishwa na yale waliojifunza nje ya nyumbani kwao.

Pamoja na hayo, tunaamini kuwa wazazi au walezi wanaweza kuchangia watoto kuingia katika vitendo visivyofaa, hivyo tunaamini kuwa kila mzazi akifanya sehemu inavyotakiwa, anaweza kusaidia kuwapo kwa maadili mema katika jamii, ambayo yatawafanya watoto wetu kuwa raia wema watakaochangia katika maendeleo ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwaka mmoja wa Rais Samia anakwenda mbali kuleta maendeleo

Na Sabato Kasika

**LEO** ndiyo Rais Samia Suluhu Hassan anatimiza mwaka mmoja tangu aapishwe kushika nafasi hiyo Machi 19 mwaka jana, akiwa amechukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuiletea maendeleo nchi.

Miongoni mwake ni kutafuta kila njia ya kuwezesha nchi inaimarika kiuchumi. Hapo akasafiri katika nchi mbalimbali, akilenga kuimarisha diplomasia ya kiuchumi, pamoja na kutafuata wawekezaji kuja nchini mwake.

Ni wazi kwamba Rais Samia, anataka kuifikisha nchi mbali hasa kwa kutumia msemo wa wahenga kwamba "Kama unataka kwenda haraka, tembea pekee yako na kama unataka kwenda mbali, nenda na wenzako."

Kwa maana hiyo, kitendo cha kuzunguka katika nchi mbalimbali na kupata mikopo ya riba nafuu, ni wazi anataka kuhakikisha nchi inafika mbali kimaendeleo, hivyo ninadhani jambo la msingi ni kumuunga mkono kwa juhudi hizo.

Kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano na mataifa mengine, Rais Samia ameshatembelea nchi kadhaa za Afrika, Ulaya na Amerika, ikiwa ni harakati za kuimarisha diplomasia ya uchumi ili kuineemesha Tanzania.

Anachukua hatua hizo kutokana na ukweli kwamba, nchi maskini kama Tanzania, njia yake pekee ya kupiga hatua ni kutumia diplomasia ya uchumi vizuri katika uhusiano na taasisi na nchi nyinginezi.

Ninaamini kuwa, wanaofuatilia kile anachokifanya, watakubaliana nami kuwa juhudi zake za kuimarisha uchumi zimemfanya atumie majukwaa ya kimataifa ili kuiweka nchi katika ramani ya utalii kupitia programu ya kimatataifa iitwayo Royal Tour. Siyo siri kwamba, katika kipindi cha mwaka mmoja, Rais ameshiriki majukwaa mbalimbali ya kimataifa yanayoweza kuleta wawekezaji kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa uchumi wa Tanzania.

Katika mwaka unaotimu leo, Rais amewezesha utiaji wa saini makubaliano ya uwekezaji wenye thamani ya Sh. trilioni 19, ambazo zinaelezwa kutarajiwa kuzalisha ajira kwa zaidi ya watu 200,000.

Ajira hizo zinatajwa kuwa ni kupitia taasisi za serikali na binafsi nchini, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kimataifa, hatua ambayo ni wazi kwamba, inaendelea kusaidia kuinyanyua Tanzania kiuchumi.

Pia viongozi wa serikali wamewahi kueleza kuwa, wakati anaingia madarakani Machi 19, mwaka jana, ukuaji wa uchumi ulikuwa umeshuka kutoka asilimia saba mwaka 2019 hadi hadi asilimia 4.8 mwaka 2020.

Hapo inatajwa sababu kubwa ya kushuka kwa uchumi wakati huo kuwa ni kutokana na janga la dunia la ugonjwa wa corona, na kwamba hadi Septemba mwaka jana, uchumi ulipanda hadi kufikia asilimia 4.9.

Vile vile mwisho wa mwaka jana, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ilitangaza kukusanya Sh. trilioni 2.5 kiasi ambacho mamlaka hiyo ilieleza kuwa ni kikubwa kilichoashiria kuendelea kuimarika kwa uchumi.

Pia Wizara ya Fedha, ilishawahi kuweka wazi kuwa, kati ya Julai mwaka jana na mwezi uliopita, serikali imeshapokea Sh. trilioni 3.1 kutoka kwa washirika wa maendeleo ukiwa ni misaada ya mikopo nafuu.

Kama ambavyo wataalamu wa uchumi wamekuwa wakisema kuwa njia pekee kwa Tanzania kupiga hatua ni diplomasia ya uchumi katika uhusiano mzuri na nchi nyingine, ninaamini ndivyo alivyofanya kwa mwaka mmoja. Wakati anatimiza mwaka mmoja, ni vyema aachwe aendelee kwenda mbali na wenzake kwa lengo la kuiletea maendeleo nchi, kwa kuwa kama alivyokariri msemo wa wahenga, "Ukitaka kwenda mbali nenda na wenzako".

Ninaamini kwamba, anashirikiana na viongozi wenzake wa mataifa mengine kuhakikisha nchi inaendelea kupiga hatua za kimaendeleo.

# Ushirika wajielekeza vita dhidi ya corona

**Na Sabato Kasika**

KATIKA kampeni za kupambana na ugonjwa wa UVIKO- 19, Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Lindi kinachoundwa na wilaya tatu za Ruangwa, Nachingwea na Liwale (RUNALI), kimeelekeza wanachama wake kupambana na vita dhidi ya ugonjwa huo kama moja ya ajenda ya mkutano wao mkuu.

Mwenyekiti wa chama hicho, Odas Mpunga, alisema jana kuwa, kwa sasa vyama vinavyounda RUNALI, kila kimoja kinafanya mkutano mkuu wa mwaka baada ya kumalizika kwa msimu wa korosho wa mwaka 2021/2022.

"RUNALI inaundwa na vyama 105 na kila kimoja kinafanya mkutano wa mwaka, tumeelekeza suala la kupambana na corona liwe ni mojawapo ya ajenda katika mikutano hiyo," alisema Mpunga.

Mpunga alisema, Ruangwa ina vyama 27, Nachingwea vyama 39 na Liwale vyama 39, ambavyo vinaendelea na mikutano ya kujadili mafanikio na matatizo yaliyojitokeza katika msimu ulioisha.

"Katika kila mkutano wa chama huwa yupo mjumbe kutoka RUNALI ambaye hupewa nafasi ya kuzungumzia umuhimu wa kujikinga na ugonjwa huo kwa kufuata maelekezo ya Wizara ya Afya," alisema.

Alisema, mara baada ya vyama vyote vinavyounda RUNALI kumaliza mikutano yake ya mwaka, utafuata mkutano mkuu wa RUNALI mwezi ujao na kwamba utaratibu utakuwa ni huo wa kuchukua tahadhari ya UVIKO19.

Alisema, yeye na wajumbe wa bodi ya RUNALI walishapata chanjo, na kwamba hawana budi kuhakikisha wanachama wa chama hicho kwa hiari yao nao wanajitokeza kupata huduma hiyo.

"Sisi si wataalamu wa afya, kazi yetu ni kuhimiza tu ili kila mmoja awe tayari kupata elimu kutoka kwa wataalamu wenyewe ili hatimaye achukue hatua za kuhakikisha anakuwa salama dhidi ya ugonjwa huo,"alisema.

Alisema, Mkoa wa Lindi siyo kisiwa kisichofikika, bali una mwingiliano na watu kutoka maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi, na kwamba wanachama wao kuchukua hatua ni jambo la muhimu.

Mpunga alisema, kwa kuwa yeye na viongozi wenzake wa chama hicho walishaonyesha mfano kwa kuchanja, hawana budi kuhamasisha wanachama wao ili kila mmoja kwa nafasi yake atafakari kisha achukue hatua sahihi.

"Kwa njia hiyo, wanachama wa RUNALI bila corona inawezekana iwapo kila mmoja atazingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ya kuvaa barakoa na kunawa mikono kwa maji tiririka na pia kutumia vitakasa mikono," alisema.

# Zungu aifagilia benki kukumbuka machinga

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Ilala jijini Dar es Salaam, ameishukuru Benki ya NMB kwa kulikumbuka kundi la wafanyabiashara wadogo nchini maarufu wamachinga na kuwasaidia kukua.

Zungu alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam jana katika ofisi za makao makuu ya benki hiyo wakati akipokea kompyuta mpakato (Laptop) tano zilizotolewa na Benki ya NMB kwa ajili ya Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA).

Baada ya kupokea vifaa hivyo Zungu alizikabidhi kwa viongozi wa SHIUMA kwa ajili ya matumizi ya kiofisi ikiwemo kuweka Kanzi Data, ili iwe rahisi kutambulika na kujua shughuli wanazofanya popote walipo nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea na kukabidhi vifaa hivyo, Zungu alisema NMB ilionyesha kwa vitendo kujali maisha ya wafanyabiashara wadogo, kwa kuwasaidia mitaji na pia kushiriki katika ukuaji wao.

"Naipongeza benki ya NMB kwa vifaa hivi, hii ni hatua kubwa na mnaonyesha wazi namna mnavyoungana na Rais Samia Suluhu Hassan kusaidia wamachinga. Sote tumeona namna Rais Samia alivyofanikiwa kuwaweka wamachinga daraja la juu, nanyi mnatembelea eneo hilohilo.

"Mbali ya misaada hii pamoja na mikopo mnayowapa wafanyabiashara wadogo, naomba niwakumbushe kuwa mikopo si suluhu ya matatizo bali Wamachinga wanahitaji elimu ya ujasiriamali.

Mara kwa mara huwa ninasema kundi la Wamachinga wakiwa milioni moja, kila mmoja akitoa Shilingi 300 kwa siku hiyo ni Sh. milioni 300, kwa mwezi ni Sh. bilioni 9.

Wanaweza kabisa kuchangia ukuaji wa uchumi wan chi," alisema Zungu.

Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi NMB, Filbert Mponzi, alisema vifaa hivyo ni mwendelezo wa makubaliano waliyoingia kati yao na SHIUMA, lengo ni kutengeneza Kanzi Data itakayowasaidia kujulikana kirahisi na kufikika.

"Tunataka Wamachinga wasajiliwe, wawe rahisi kufikika. Tunashukuru Naibu Spika Zungu aliliona hili akaamua kutushirikisha, leo hii tumekabidhi kompyuta mpakato tano zenye thamani ya shilingi milioni 7.5," alisema Mponzi.

Alisema pamoja na makabidhiano ya vifaa hivyo, NMB imeendelea kushirikiana na kundi hilo la wafanyabiashara wadogo tangu mwaka 2000. Kwa wastani, benki ya NMB hutoa mikopo ya thamani ya Sh, bilioni 50 kila mwezi kwa kundi hilo la wafanyabiashara wadogo wakiwemo Wamachinga.

Katibu wa wamachinga Kariakoo, Thabit Maloka aliyemwakilisha Mwenyekiti wa SHIUMA Taifa, alisema wamepata faraja kubwa kwa msaada huo kutoka NMB, wanaamini hayo ni matunda ya Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na ahadi aliyowapa ya kuwashika mkono.

"Hatujawahi kuthaminiwa kwa kiwango hiki, tumefarijika sana kwa msaada huu wa vitendea kazi kutoka NMB, kwa sasa wamachinga watajuana kwa majina, maeneo na aina ya biashara tunazofanya na hata itakuwa rahisi kupeana ushauri na misaada mingine," alisema Maloka.

Alibainisha kuwa wanaamini huo ni mwanzo tu, kwani wanajua mazuri yanakuja. Aliuomba uongozi wa NMB kufikiria kuongeza msaada zaidi ikiwemo kufanya ukarabati wa majengo ya ofisi zao za Ilala jijini Dar es Salaam pamoja na kuwapa mafunzo ya ujasiriamali.


MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

PONGEZI

MWAKA 1 MADARAKANI



Mhe.Samia Suluhu Hassan

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

#Samia 365

1. Kusajili dawa 724 ,vifa tiba 305 na vitendanishi 138 baada ya kujiridhisha na ubora, usalama na ufanisi wake
2. Kuendelea kushikilia cheti cha ithibati cha ISO 9001:2015 na ithibati kwa Maabara kiwango cha ISO/IEC 17025:2005
3. Kuongeza bajeti kulikowezesha utoaji huduma kwa ufanisi na kutoa gawio kwa Serikali kiasi cha Tsh bilioni 5.9
4. Kuendelea kutoa msaada wa kiufundi kwa viwanda vipya 15 vya dawa na 24 vya vifaa tiba nchini
5. Kuidhinishwa kwa Muundo wa TMDA na ongezeko la Watumishi kufikia 293
6. Matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika utoaji huduma za vibali ambapo sasa vinatolewa ndani ya saa 24
7. Kuendelea kushikilia ngazi ya Tatu ya WHO ya ubora wa mifumo ya udhibiti(Maturity Level 3)
8. Kusogeza huduma kwa wananchi kwa kujenga ofisi ya kanda ya kati
9. Kuanzishwa kwa Maabara za tumbaku na dawa za mitishamba mkoani Dodoma na Maabara ya vitendanishi jijini Dar es Salaam

"TMDA Hulinda Afya ya Jamii"

0800110084 @tmda_tanzania @tmda tanzania www.tmda.go.tz

# Wateja Tigo kuvuna mapesa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya utoaji wa huduma za kidigitali nchini Tigo Tanzania, kupitia mfumo wake wa huduma za kifedha wa Tigo Pesa, imezindua promosheni mpya ya wiki tano inayojulikana kwa jina la "Pesa Mwaa Mwii na Tigo Pesa".

Promosheni hiyo itawawezesha wateja wa Tigo Pesa kuondoka na zawadi za fedha taslimu hadi Sh. milioni 325.

Kwa mujibu wa Tigo, promosheni hiyo inatokana na mafanikio ya ofa ya Tigo Pesa ya kutimiza miaka 10 iliyozinduliwa mwaka jana ili kuwahimiza wateja kutumia suluhu za malipo ya kidijitali katika miamala yao ya kila siku.

Taarifa ya Tigo ilisema wateja wa Tigo Pesa wanastahili kuingia kwenye droo na kujishindia zawadi za fedha taslimu kwa kufanya miamala tofauti tofauti kama vile Lipa Kwa Simu, Malipo ya Bili, Malipo ya Serikali, miamala ya mtandaoni na kupokea pesa kutoka kwa mtandao mwingine wa simu.

"Tigo Pesa kwa miaka mingi imechangia katika ajenda ya kitaifa ya ujumuishi wa kifedha na kupitia bidhaa na huduma zetu za kibunifu zinazomlenga mteja tumefikisha huduma thabiti za kifedha kwa zaidi ya wateja milioni tisa, alisema Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, wakati wa uzinduzi wa promosheni hiyo.

"Tumeona ukuaji wa utegemezi wa huduma za kifedha kwa simu za mkononi nchini kote na promosheni ya Pesa Mwaa Mwii na Tigo Pesa inajikita katika dhamira yetu ya kukuza malipo ya kidijitali nchini kote kwa kutumia suluhu mbalimbali za kidijitali zinazowezesha watumiaji katika ulimwengu unaozidi kuwa wa kidijitali," aliongeza.

Pia alisema promosheni hiyo ya 'Pesa Mwaa Mwii na Tigo Pesa' ni maalum kwa wateja wa Tigo Pesa na kwamba kupitia promosheni hiyo, kutakuwa na washindi 111, kati yao 20 wakishinda milioni kila wiki kwa wiki tano na washindi 10 kupata zawadi mwisho wa promosheni huku mshindi wa jumla akipata Sh. milioni 25.

Ili kushinda, alisema wateja wanahimizwa kufanya miamala mingi iwezekanavyo kutoka kwa huduma zilizotajwa hapo juu ili kupata nafasi ya kuwa mamilionea.

# Mafanikio 15 ya MNMA mwaka 1 wa Samia

**Na Romana Mallya**

CHUO cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) kimetaja mafanikio 15 ambayo wameyafanya katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan tangu alipoingia madarakani.

Mojawapo ni kukamilisha kuandaa mitaala mipya na kuihusisha ya zamani na kuliingiza somo la uongozi maadili na uzalendo katika mitaala yote.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila alieleza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia na waharirí na waandishi wa habari.

Alisema wameingiza somo hilo katika mitaala ili kila mwanafunzi apate ufahamu wa kutosha kuhusu uongozi, maadili na uzalendo.

Prof. Mwakalila alisema sera ya udhibiti ubora imehuishwa ili kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa ni bora na yenye viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

"Chuo kimetenga bajeti kwa ajili ya kuwawezesha wahadhiri kufanya utafiti wenye maslahi kwa chuo na wamejengewa uwezo wa kuandika maandiko ya utafiti na machapisho," alisema.

Pia alisema chuo kinatoa mafunzo ya uongozi na maadili kwa viongozi na watendaji kutoka taasisi mbalimbali pamoja na wanafunzi wa chuo na kufanya idadi ya waliofuzu kuwa zaidi ya 4,000.

Alitaja mafanikio mengine ni uboreshaji wa miundombinu kampasi ya Kivukoni kwenye mabweni, madarasa na ofisi ikiwa ni pamoja na kuweka umeme jua na kuboresha barabara za ndani.

Kadhalika, alisema katika kampasi hiyo mshauri elekezi kwa ajili ya ujenzi wa maktaba kubwa yenye uwezo wa kuchukua zaidi ya watu 2,500 pamoja na ukumbi wa mihadhara utakaochukua watu 1,000 ameshakamilisha michoro yake na mchakato wa kumlata mkandarasi unaendelea.

Alisema kwa upande wa tawi la Pemba, mshauri elekezi tayari ameshaandaa mpango wa eneo la chuo, usanifu wa majengo kwa ajili ya madarasa, mabweni na jengo la utawala.

Prof. Mwakalila alisema kampasi ya Kivukoni imeongeza udahili kutoka wanafunzi 9,754 mwaka 2020/21 hadi 11,184 mwaka 2021/22 na idadi ya wahitimu imeongeza kutoka 3,154 mwaka 2019/20 hadi 4,330 mwaka 2020/21.

"Chuo kimewezesha wahadhiri 56 kwenda kwenye mafunzo kwa ngazi ya Shahada ya uzamivu, shahada ya uzamili, shahada ya awali na stashahada. Idadi ya wahadhiri wenye Shahada ya Uzamivu imeongezeka hadi 40.

Prof. Mwakalila alisema ndani ya mwaka mmoja wa Rais Samia amewezesha kujenga uhusiano wa Taifa na nchi nyingine duniani kwa sababu Tanzania siyo kisiwa.

"Lazima tufahamu kwamba misingi iliyojengwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ilikuwa misingi ya kuleta uhusiano na mataifa mengine. Katika sekta ya elimu zipo jitihada zilizofanyika katika ujenzi wa madarasa, pia tumeshuhudia utulivu amani na furaha Kwa Watanzania na limechochea maendeleo," alisema.

Kaimu Naibu Mkuu wa Chuo (Utawala, Fedha na Mipango), Ukende Mkumbo, alisema mwaka mmoja wa Rais Samia amedhihirisha kuwa mwanamke siyo kigezo cha kuwa legelege bali ni mjenzi wa Taifa na amefanya nchi kutulia na kuruhusu watu kufanya kazi.



Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shedrack Mwakalila (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu chuo hicho, kufungua tawi katika Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi. Kulia ni Kaimu Mkuu wa Chuo hicho (Mipango na Fedha na Utawala), Ukenda Mkumbo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SUA kuwanoa waganga tiba asili

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia mradi wa VaSPHARD kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kimeendesha mafunzo kwa waganga wa tiba asili ya kisha kupima dawa zao ili kubadilisha mtazamo na tabia katika kuzalisha dawa.

Lengo la kufanya hivyo ni kuwawezesha wataalamu hao wa tiba asilia kutengeneza dawa salama, safi na zenye viwango vya juu na kupata usajili.

Mkuu wa Mradi wa VaSPHARD, Dk. Faith Mabiki, alisema mafunzo hayo yaliwakutanisha waganga wa tiba asili na watengenezaji wa dawa 35 kutoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania ambao wamekuja na zaidi ya dawa 100.

Alisema baada ya majadiliano na kujengeana uelewa, dawa hizo zitapimwa na kisha kupewa majibu kujua ubora na kuwashauri namna bora za kuzalisha na kufungasha ili kukidhi viwango vya kimataifa.

"Kwa hiyo sasa hivi tunajadiliana nao baada ya kuwajengea uelewa, tunaingia nao makubaliano kisha tutakwenda maabara kufanya vipimo viwili ambavyo vimewekwa na serikali ili kutengeneza dawa kiusalama zaidi," alisema Dk. Mabiki.

Alisema ili serikali izitangaze dawa hizo, lazima wapelekwe kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kuangaliwa vipimo kadhaa kama vile sumu kuvu, vipimo vya wadudu wanaosababisha magonjwa au dawa kuwa chafu, vipimo vya madini tembo na kemikali iliyo ndani ya dawa.

"Kwa bahati nzuri vipimo hivyo vyote SUA tunaweza kuvifanya ndiyo maana Mkemia Mkuu wa Serikali ametupa kufanya baada ya kupata fedha kutoka Jumuiya ya Wanataaluma wa Sayansi Afrika," alisema.

Mtaalamu wa tiba asili kutoka Njombe, Flavian Nyakeji, alisema wamefurahi kupata nafasi hiyo ya kipekee ya kuelimishwa na kujua namna ya kutengeneza dawa zenye ubora.

Alisema ameleta dawa 10 kwenye mchakato huo ili kujua nini kimo kwenye dawa zake hasa kwa kujua ubora na yuko tayari kupata ushauri wa kitaalamu wa namna ya kuboresha dawa hizo ili kuwa na viwango badala ya kuzalisha bila viwango hali ambayo itatunyima usajili na kutofikia soko la nje.

# RC aunda kamati kukagua eneo ujenzi sekondari

**Na Frank kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, ameunda kamati ya watu saba kwa ajili ya kukagua eneo la kujenga Sekondari ya Kata ya Homboza, iliyopo wilayani Mvomero baada ya eneo la awali lililokuwa limekubaliwa kuwa sio salama.

Shigela alilazimika kuunda kamati hiyo wakati akikagua matumizi ya fedha zaidi ya Sh. milioni 470 zilizotolewa na serikali na kutofanyiwa kazi kwa zaidi ya miezi miwili kwa sababu ya mivutano ya wapi shule hiyo ijengwe.

Alisema baada ya kufika Kijiji cha Manza, eneo ambalo shule inatakiwa kujengwa, alijiridhisha kuwa hakuna mgogoro wowote wa ardhi na kama kuna mwananchi ana mgogoro na eneo hilo aende mahakamani.

"Yako maeneo saa yote ni mgogoro tu, hata ardhi isiokuwa na mgogoro wanataka watengeneze mgogoro na wengine wanataka ardhi sio kwa ajili ya kujiendeleza, wanataka wachukue ili wakauze kwa watu wengine kwa hiyo suala la ardhi tumefunga, Kamishna wa Ardhi kama kutatokea mgogoro mwingine mwambie aende mahakamani," alisema Shigela.

Alisema kamati aliyoiunda itaenda kukagua eneo ambalo limekubaliwa na wananchi kujenga shule ya sekondari baada ya awali kuonekana kutofaa kwa kuwa ni chepe chepe na hatarishi kwa wanafunzi watakaosoma shuleni hapo.

Aliwataja wajumbe hao pamoja na Ofisa Elimu wa Mkoa wa Morogoro, Ofisa Mazingira wa Mkoa, Kamishna wa Ardhi wa Kanda ya Mashariki na Ofisa Elimu wa Wilaya ya Mvomero.

Wengine ni Ofisa Tarafa ya Mlali na Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Mvomero, wote wameagizwa kuambatana na Diwani wa Kata ya Homboza, Hamidu Kalungwana, kupitia eneo ambalo wananchi wameliteua kuwa mbadala wa eneo la awali ili kuona endapo eneo hilo linafaa kwa ujenzi huo na kama halitafaa kamati hiyo itafute eneo lingine lisilo na mgogoro.

Kwa upande wake diwani wa kata hiyo, Mamidu Kalungwana, alithibitisha kuwa eneo hilo halina mgogoro na uvumi kuwa eneo hilo lina mgogoro uliotungwa na baadhi ya wananchi wasiotakiwa mema serikali yao ambao muda wote wanatamani kuchochea vurugu.

# Bil. 174/- kukamilisha vyuo vya umahiri

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

WIZARA ya Elimu inatarajia kutumia zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 75 (Sh. 174,431,585,606) kukamilisha ujenzi wa vyuo vya umahiri vilivyoko katika kanda mbalimbali nchini kwenye mikoa ya Arusha na Dodoma.

Naibu Waziri wa Elimu, Dk. Omari Kipanga, aliyasema hayo alipokuwa akitembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa majengo ya Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kinachojengwa katika Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida. "Rais ametoa Dola milioni 75 za Kimarekani kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya umahiri ambavyo vimejengwa katika kanda mbalimbali," alisema.

Alisema, Kanda ya Arusha watajenga chuo cha umahiri katika uzalishaji au ufundishaji wa wataalamu sekta ya uzalishaji wa umeme wa kutumia maji mkoani Arusha.

Kadhalika chuo kingine kikubwa kinajengwa Dodoma na asilimia 40 ya ujenzi umekamilika, zaidi ya Sh. bilioni 17.9 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho mkoani humo.

Alisema mkoani Mwanza kitajengwa Chuo cha DIT kitakachoshughulika na uongezaji thamani ya ngozi nao baada ya ujenzi huo kukamilika watafundishwa wataalamu wa sekta ya ngozi wakati kwenye Chuo cha DIT kilichoko mkoani Dar es Salaam kitakuwa ni kituo cha masuala ya TEHAMA.

Alisema wizara hiyo imepokea zaidi ya Sh. bilioni 20 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika mikoa ya Simiyu, Geita, Njombe pamoja na Rukwa ili kuhakikisha mikoa yote 25 ya Tanzania Bara inakuwa na vyuo hivyo.

Alifafanua katika fedha za UVIKO-19 zilizopokelewa Oktoba, mwaka jana, zaidi ya Sh. bilioni 64 zilizopokelewa, Sh. bilioni 20 zilielekezwa kwenda kukamilisha ujenzi wa vyuo vyote vya ufundi.

Katika sekta ya elimu alisema kwa ujumla walipatiwa zaidi ya Sh. bilioni 304 na dhamira kuu ni kuhakikisha watoto wote walioko katika mikoa 25, ifikapo Juni, mwaka huu wanakuwa darasani wakiendelea na masomo yao. Mpaka sasa alisema, Wizara ya Elimu imeshapokea zaidi ya Sh. bilioni 8.7 kwa ajili ya kununua thamani ili vyuo hivyo vitakapokamilika watoto waanze kupata masomo katika majengo hayo na kutokuwa na ukosefu wa vifaa vya kusomea na kujifunzia.

Akitoa taarifa za maendeleo ya mradi huo wa ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya Ikungi mkoani Singida kwa Naibu Waziri wa Elimu, Mkurugenzi Mkuu wa VETA, alimhakikishia Naibu Waziri kwamba wamejipanga kikamilifu kuhakikisha chuo hicho kinakamilika kwa wakati uliokusudiwa.

Alisema maagizo yaliyotolewa na Naibu Waziri ni pamoja na kuwa na mpango kazi kwa kila jengo, ununuzi wa vifaa vya mradi wa ujenzi huo, kuwe na mikataba na mafundi pamoja na kuwa na genge la mafundi wa kila jengo.




Ofisa Mkuu wa Ubunifu na Mikakati wa Bidhaa za Tigo, David Umoh (kulia), akipongezana na Mkurugenzi Mkuu wa Samsung Afrika Mashariki, Tae Sun Lee, baada ya kuzindua huduma ya intaneti majumbani kwa watumiaji wa televisheni zote Smart za Samsung, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji watangaziwa kiama wizi wa kaboni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama imetangaza kiama kwa wachimbaji wadogo wanaojihusisha na vitendo vya wizi wa kaboni zinazosadikiwa kuwa na madini ya dhahabu na kusababishia serikali kuendelea kukosa mapato.

Imesema pia, mchimbaji atakayebainika kutorosha kaboni hizo atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufutiwa leseni yake ya uchimbaji kwa sababu atakuwa mhusika moja kwa moja katika kuikosesha serikali mapato kupitia madini.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo makundi mbalimbali ya wachimbaji wadogo namna bora ya kufanya shughuli zao katika hali ya usalama yaliyoendeshwa na Tume ya Madini.

Alisema, serikali inataka kila mchimbaji mdogo apate haki yake kwa kile ambacho atakuwa amekitumikia na kama kuna wachimbaji wenye tabia hiyo katika maeneo yake ni bora akaache kujishughulisha na wizi huo ambao upo kwa sasa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na hapo awali. Alisema, serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kuwa wanaojihusisha na tabia hiyo ya wizi wa kaboni wanatafuta kazi zingine za kufanya ili waweze kujiingizia kipato chao kwa kuwa watakapobainika wataondolewa katika maeneo ya uchimbaji na watakuwa hawana nafasi ya kufanya shughuli hizo tena.

Ndanya alisema, mafunzo hayo yatakwenda sambamba na usalama mahali pa kazi, usimamizi wa baruti, uendeshaji wa mitambo ya uchenjuaji pamoja na sheria za madini ambazo zimekuwa zikifanyiwa marekebisho mara kwa mara.

Aliwataka wachimbaji wadogo kuzingatia taratibu za uchimbaji wa madini ambazo zipo ili kuepukana na ajali kazini na kujenga utaratibu wa kutoa taarifa kwa viongozi juu ya wachimbaji ambao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya wizi na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Awali akitoa taarifa ya makusanyo ya maduhuli ya serikali, Ofisa Madini Mkazi mkoa wa kimadini Kahama, Mhandisi Jeremiah Hango, alisema mwaka 2021/2022 walikusanya Sh. bilioni 95 ambazo ziliongezeka kutoka Sh. billioni 79 kwa mwaka 2020/ 2021 licha ya mgodi mkubwa wa Buzwagi kufungwa.

Alisema, hadi kufikia Februari 28, mwaka huu walikuwa wameshakusanya maduhuli ya serikali Sh. bilioni 69.81 sawa na asilimia 110 ya lengo la kipindi husika ya asilimia 73.48 la mwaka wa fedha 2021/2022 na jumla ya tani 2.3 za madini ya dhahabu zilipelekwa sokoni.

Hango alisema, jumla ya dhahabu yenye kilogramu 1,564.83 yenye thamani ya Sh. bilioni 178.23 iliuzwa katika masoko ya dhahabu kwa kipindi cha Julai mosi, mwaka 2021 mpaka Februari 2022, mrabaha na ada ya ukaguzi ilikuwa Sh. bilioni 12.48 huku kodi ya huduma ikiwa Sh. milioni 534.70.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Migodi na Mazingira kutoka makao makuu, Mhandisi Henry Mditi, alisema nia ya mafunzo hayo ni pamoja na kuhakikisha wachimbaji wanafanya kazi zao katika hali ya usalama wakati wote wawapo kazini.

Alisema kuwa mafunzo hayo yamekuwa yakiendelea katika maeneo mbalimbali nchini na hawapaswi kuona kuwa wachimbaji wanapoteza maisha kwa ajili ya kupigania uchumi wa nchi na wakati wanauweza wa kuwafikia na kuwapatia elimu ya usalama mahala pa kazi.

# Dangote kusafirisha tani 43,000 saruji nje

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MAMLAKA ya Bandari Nchini (TPA), imekabidhi hati ya kibiashara kiwanda cha kuzalisha saruji cha Dangote mkoani Mtwara, itakayoiwezesha kusafirisha tani 43,000 za saruji kwa mwezi kutoka Bandari ya Mtwara, Dar es Salaam na Tanga kwenda nje ya nchi.

Kaimu Meneja Masoko wa Bandari, Lydia Malya, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Bandari nchini, Eric Hamissi, akikabidhi hati hiyo, alisema kabla ya makubaliano hayo Dangote walikuwa wakisafirisha tani 13,000 kwa mwezi kutoka Bandari ya Mtwara kwenda Zanzibar na Comoro.

Alisema majadiliano ya kuifanya Kampuni ya Dangote, kutumia bandari za TPA kusafirisha mizigo yake yalianza Juni, mwaka jana kabla ya kufikiwa muafaka mapema mwaka huu.

"Lengo la makubaliano haya ni kuongeza tija kwa pande zote na sisi Bandari baada ya makubaliano haya tutakuwa tumeongeza shughuli zitakazokuwa zinafanyika katika bandari zetu na watu wetu wanaofanya shughuli mbalimbali bandarini," alisema Malya.

Alisema kabla ya makubaliano hayo, Dangote walikuwa wakitumia Bandari ya Mtwara kusafirisha wastani wa tani 13,000 kwenda Zanzibar na Comoro.

Meneja wa Bandari Mtwara, Norbet Kalembwe, alisema makubaliano hayo yatasaidia kupunguza uharibifu wa miundombinu ya barabara kwa kuwa kiasi kikubwa cha saruji kilichokuwa kinasafirishwa kwa njia ya barabara kitasafirishwa kutumia njia ya maji.

Makubaliano hayo yatatoa fursa mbalimbali kwa wakazi wa Mtwara ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa ajira kupitia bandari hiyo kwa kile alichoeleza mizigo yote kwenda katika bandari zingine itaanzia kwenye Bandari ya Mtwara.

"Hii ni fursa mpaka kwa wakazi wa Mtwara, kwani nguvu kazi itahitajika tofauti na awali tulipokuwa tukisafirisha kiasi kidogo cha saruji, lakini itaongeza tija kwenye bandari yetu na kukuza uchumi wa nchi," alisema Kalembwe.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kiwanda cha Dangote, Abdullahi Baba, akizungumza baada ya kupokea hati hiyo, alisema kwa kiasi kikubwa watapunguza gharama walizokuwa wakitumia wakati wa usafiri wa njia ya barabara.

Aliongeza kuwa kwa sasa wana nafasi kubwa ya kuyafikia masoko mengine ya nje kwa kutumia bandari za TPA, ikiwamo masoko ya nje ya nchi waliyokuwa wakilazimika kuyafuata kwa njia ya barabara.

Alisema mwanzo walikuwa wanapata shida kushindana kwenye masoko ya ndani kutokana na kusafirisha bidhaa zao kwa umbali wa zaidi ya kilometa 600 kutoka Mtwara.

"Ukiangalia sisi tunazalisha tukiwa huku mbali tunasafirisha kwenda mikoa tofauti, lakini kwanza ni lazima tusafiri zaidi ya kilometa 600, walipo wazalishaji wengine, naamini kwa utaratibu huu tunaweza kushindana na hata wakati mwingine tukawa na bei nafuu zaidi kwenye bidhaa zetu zinapoingia sokoni," alisema Baba.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliyekuwa mgeni rasmi katika tukio hilo, alisema mafanikio ya Dangote katika uwekezaji nchini, yatawavuta na wawekezaji wengine na kuinua hali ya uchumi wa taifa.

Alisema serikali baada ya kuwekeza Sh. bilioni 157 kwa ajili ya maboresho ya Bandari ya Mtwara, Rais Samia Suluhu, alitoa maelekezo ya kuhakikisha bidhaa zote zinazoingia na kutoka katika ukanda wa kusini zipitie Bandari ya Mtwara.




Rais wa Rotary Eklabu ya Masaki, Akshay Vithlani (kulia), pamoja na Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (wapili kulia), wakishirikiana na wana Rotariani kukabidhi msaada wa viatu kwa baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Bunge, jijini Dar es Salaam jana. Eklabu imetoa jozi za viatu 372 kwa ajili ya wanafunzi hao. Watatu kushoto ni Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Leonida Mulekuzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani wapinga uamuzi wa kuondoa magari madogo stendi

**Na Happy Severine,** BARIADI

MADIWANI wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu, wameendelea kupinga uamuzi uliofanywa na Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lupakisyo Kapange, pamoja na kamati kuu ya siasa ya wilaya kwa kuondoa magari madogo ya abiria (Mchomoko) ndani ya stendi kuu (Somanda), hali iliyosababisha halmashauri hiyo kushuka kimapato.

Maamuzi hayo ambayo madiwani wameendelea kulalamikia ni kuyaondoa magari madogo yaliyokuwa yakipaki ndani ya stendi hiyo na kuyaruhusu kuingia katikati ya mji wa Bariadi na kuegesha eneo la sokoni ilipokuwa stendi ya zamani.

Wamesema kuwa kitendo hicho kilichofanywa na Mkuu huyo wa wilaya na kamati ya siasa ni kuingilia mamlaka ya halmashauri na kimefanywa kisiasa zaidi bila kuzingatia maslahi ya serikali.

Madiwani hao walisema wanashangazwa na uamuzi huo kwa kuwa lengo kuu la kujengwa kwa stendi hiyo ya Somanda ni kuhudumia mabasi makubwa na madogo ya abiria yaendayo nje na ndani ya mkoa huo.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya mji wa Bariadi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Kija Bulenya, alisema stendi ya Somanda imejengwa kwa lengo la kuhudumia mabasi pamoja na kuiingizia halmashauri mapato kupitia ushuru wa mabasi hayo, lakini kwa sasa yameendelea kushuka kwa kasi kutokana na uamuzi uliofanyika bila kushirikishwa wao na wataalamu wa serikali.

Vilevile, alisema hapo awali kabla ya kuhamishwa kwa magari hayo, halmashauri hiyo ilikuwa ikikusanya kiasi kikubwa cha fedha kuanzia Sh. milioni 28 hadi Sh. milioni 25 kwa mwezi, lakini kwa sasa yameshuka na kufikia milioni 15.

Samola Nola, Diwani wa Kata ya Buhnamala, alisema stendi ya Somanda imetumia Shilingi bilioni saba hadi kukamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia na itashangaza kama miundombinu iliyojengwa haitatumika kuipatia mapato halmashauri.

# DC azionya kamati za maji ubadhirifu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amezionya kamati za maji kutofanya ubadhirifu wa fedha kwenye miradi ya maji, ambayo imetekelezwa kwenye vijiji vyao kuwa fedha wanazozikusanya za mauzo ya maji wazipeleke benki na sio kukaa nazo na kuzitafuna.

Mboneko alibainisha hayo juzi wakati alipofanya ziara ya kukagua baadhi ya miradi ya maji wilayani Shinyanga, ambayo inatekelezwa na wakala wa maji vijijini (RUWASA), kuwa miradi mingi imekamilika na kuanza kutoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi na kutaka kuona miradi hiyo inadumu kwa muda mrefu.

Alisema hataki kusikia fedha za mauzo hayo ya maji zinakaa majumbani, bali zipelekwe benki kuhifadhiwa ili kusije tokea tatizo la ubadhirifu wa fedha hizo na kusababisha miradi kukwama kuhudumia wananchi baada ya kushindwa kujiendesha kutokana na ukosefu wa fedha za kulipia bili za maji na matengenezo ikiharibika.

"Nimekagua miradi mingi ya maji na yote inatoa huduma, pongezi nyingi ziende kwa RUWASA, kwa kuzitumia fedha hizi vizuri za miradi ya maji ambazo zilitolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Maji, na ndiyo kiu kubwa ya Rais kuona wananchi wanapata majisafi na salama," alisema Mboneko.

"Kwenye usimamizi wa miradi hii ya maji nazionya kamati katika maeneo yote wilayani Shinyanga, sitaki kusikia kuwapo na ubadhirifu wa fedha za mauzo, mtazitapika hizo fedha sitaki miradi hii ikwame kuhudumia wananchi sababu ya kuendekeza matumbo yenu, nataka fedha zote ziwe zinapelekwa benki," aliongeza.

Aliwataka pia watu ambao wateuliwa kusimamia kuuza maji kwenye vituo vya maji, wawe waaminifu pamoja na kuwapo muda wote vituoni ili wananchi wapate huduma stahiki ya majisafi na salama na sio wakuanza kutafutwa, na hatimaye wananchi kurudi kutumia maji yasiyofaa tena kiafya.

Katika hatua nyingine, aliwataka wananchi waitunze miundombinu ya miradi hiyo kusiwapo na wizi wa mabomba ili iendelee kuwahudumia vizazi na vizazi na kuondokana na adha ya kufuata maji umbali mrefu au kutumia ya kwenye mabwawa ambayo sio salama.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Edward Ngelela, alipongeza utekelezaji wa miradi ya majisafi na salama kwa wananchi na kubainisha kuwa huo ndiyo utekelezaji wa ilani ya chama hicho kwa vitendo.

Baadhi ya kinamama, Rebeka Mpuya na Jesca Masanja, kwa nyakati tofauti walisema huduma hiyo kuwa karibu imewaondolea adha ya kufuata maji umbali mrefu na kutougua magonjwa.




Idara Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inavyobeba hadhi mdau wa tija serikalini




Hili la Russia vs Ukraine linatufunza nini masikini?


# BUFE

IJUMAA MACHI 18, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA





**Staili ya uchumi wa Rais Samia, ina nuru leo, matarajio kesho**

## MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA

# Kinamama wakutana Dar na kumpongeza, wakijipanga zaidi

• Waainisha mianya yao ya maendeleo

**Na Yasmine Protace**

HARAKATI za wanawake kushika nafasi za juu katika uongozi zina historia ya miaka mingi na kadri muda unavyosonga, ndivyo mafanikio yanavyoshuhudiwa, kipindi kilichoko kikiwa marejeo makuu.

Katika kupigania harakati hizo matunda yameonekana kwa kushuhudiwa viongozi wa nafasi za juu wanawake kuwa na ushindi mkubwa katika kiti hicho cha kileleni. Ni hali inayotoa ishara bado mapambano ya wanawake kusaka uongozi kunaonyesha nuru njema ya ufanisi.

Hivi karibuni, wanaharakati wametoa pongezi zao kwa Rais Samia Suluhu Hassan, wakitambua mchango wake katika kuleta maendeleo. Sasa ni dhahiri kunashuhudiwa hata katika safu ya utendaji kiserikali, kumekuwapo ongezeko la wanawake katika uongozi.

Ni hatua inayochukua nafasi yake, kesho ikiwa kilele unatimia mwaka mmoja madarakani, akiwa katika ulingo wa mafanikio ya mwaka mmoja madarakani.

Balozi Mstaafu Nyasugara Kadege, anazungumza katika maadhimidho ya Siku ya Wanawake Duniani katika hafla iliyoandaliwa na taasisi ya TGNP Mtandao, akitumia umri na uzoefu wake kazini kufafanua mantiki iliyopo, kwamba serikali sasa inawatambua . Alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla hiyo .

"Serikali ya Awamu ya Sita kumekuwa na ongezeko la wanawake katika uongozi," anasema Balozi Kadege, akisifu hatua ya TGNP Mtandao kuzindua mfumo wa kazi data, utazisaidia mamlaka za serikali kutambua wanawake kuzifahamu kazi zao wanazozifanya.



Mkuu wa Nchi, Samia Suluhu Hassan, alipokutana na kinamama katika hafla iliyofanyika katika ukumbi wa taasisi ya TGNP Mtandao, Dar es Salaam, wakati huo akiwa Makamu wa Rais. **PICHA: MAKTABA**

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, anasema kazi data wakiwa nayo itawasaidia wanawake kujitambua, kwani huwa mtu anaandaliwa kuanzia umri mdogo na katika muundo wa maisha ni vigumu kumtenganisha mwanamke na uwekezaji.

Anasema, suala la usawa wa kijinsia ni la maendeleo na wanawake wasiposhiriki kikamilifu, kunawachangia kurudi nyuma kimaendeleo na mara zote, vikwazo vinavyomrudisha nyuma mwanamke ni kutokuwapo usawa katika maendeleo.

Gema Akilimali ni mwenyekiti wa sasa wa TGNP Mtandao, akisema pamoja na kuwapo siku ya harakati za kumkomboa mwanamke, bado kuna kinamama wameachwa nyuma ilhali ni wazalishaji wakubwa.

Mwanaharakati wa haki za kinamama, Shamim Khan, anasema wanaume, wanatakiwa kuwasaidia wanawake katika maendeleo ili wasiteseke.

Palagia Kijuu, ni mwakilishi kutoka asasi ya wanawake ya Umoja wa Mataifa nchini (UN Women), ana maoni yake katika hafla iliyofanyika viwanja vya Mabibo jijini Dar es Salaam, anafafanua: "Tanzania bado inakabiliwa na mfumo dume na mila kandamizi na hali hiyo imekuwa ikisababisha wanawake kuzidi kukandamizwa."

Ofisa huyo wa UN Women anaongeza kwamba, sauti zinapaswa kuendelea kupazwa kuzuia mila kandamizi na mfumo dume, ili kuwezesha kumtoa mwanamke asiendelee kukandamizwa zaidi, huku akiahidi ifikapo mwaka 2030 kunatakiwa kung'olewe mizizi yote inayowakandamiza wanawake.

"Mfumo wa sheria tunataka usimamie, ili kumkomboa mwanamke ili asibaki nyuma," anasema Palagia.

Mwakilishi kutoka ubalozi wa Norway nchini, Anette Otille anatoa uzoefu wake, kwamba nchi yao ina kawaida kuwashirikisha wanaume katika kukuza usawa wa kijinsia, ikizingatia mamlaka makubwa aliyonayo mwanaume katika familia.

Anasema katika miaka 15 iliyopita, maazimio yalikuwa ni kuhakikisha asilimia 45 ya kampuni zote duniani, ziwe na wanawake katika nafasi za juu.

Kwa mujibu wa ofisa huyo wa ubalozi, nchi yao Norway hivi sasa ipo tayari kushirikiana na Watanzania katika kuleta mageuzi ya usawa wa kijinsia kitaifa.

MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA

# Idara Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inavyobeba hadhi mdau wa tija serikalini

• Mpango mkakati kutoka maagizo ya Rais • Ofisi matawi, teknolojia kidigitali kitaifa • Mtaji mpya wa nyaraka, fikra za waasisi taifa

**Na Mary Mwakapenda**

KUMBUKUMBU na nyaraka mara zote zinajulikana kuwa nyenzo muhimu, katika utendaji kazi serikalini na taasisi zake. Bila ya kuwa na kumbukumbu na nyaraka sahihi, hatuwezi kujua tunakotoka na tunakokwenda hata tunashindwa kufikia uamuzi sahihi kwa wakati. Kumbukumbu na nyaraka huwa zinatumika kama kielelezo cha uwajibikaji na nguzo muhimu katika utawala bora.

Kutokana na umuhimu wa kumbukumbu na nyaraka, serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, imeiwezesha Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na utunzaji nyaraka muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Uwezeshaji huo unatajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye ufanisi wa serikali, ni mafanikio kwenye eneo la utunzaji kumbukumbu na nyaraka za taifa katika kipindi cha mwaka mmoja.

Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za utendaji (keyword filing system) na mahsusi Mfumo wa Masijala Mtandao (e-File Management System) katika taasisi za umma, ambako ufanisi na tija katika utoaji huduma serikalini, umeongezeka kwa kiasi kikubwa.

Idara hiyo imeendelea kukusanya nyaraka kutoka katika taasisi za umma zenye umuhimu na kuziweka katika hifadhi salama na mifumo wezeshi, kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wake pale zinapohitajika, kwa ajili ya rejea serikalini, ili kuwezesha kufanyika uamuzi sahihi na kwa wakati.

Ni hatua inayosaidia kutambua kumbukumbu muhimu kama 'Urithi Andishi wa Taifa' kwa ajili ya kuhifadhi historia ya nchi, kusaidia ufanyaji utafiti mbalimbali na kurahisisha marejeo, pale zinapohitajika ili kuwezesha kufanyika uamuzi sahihi na kwa wakati.

### WAJIBU WAKE ULIKOJIKITA


Kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ya mwaka 2002 na Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa ya mwaka 2004, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, imepewa mamlaka kusimamia na kuratibu shughuli za utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma.

Katika hili inawajibika kushauri, kuratibu na kusimamia mifumo ya utunzaji kumbukumbu katika taasisi za umma, pia ikiwa na jukumu la kubaini, kukusanya na kuhifadhi nyaraka ambazo ni urithi andishi kwa lengo la kuhifadhi historia ya Taifa letu. Aidha, idara hiyo inawajibika na kuelimisha na kuhamasisha umma ndani na nje ya nchi, kuhusu nyaraka ili wazitumie katika utafiti mbalimbali.

Eneo lingine inalowajibika nalo ni katika kukarabati nyaraka kongwe na kuziweka katika mifumo ya kidigitali, ili kurahisisha upatikanaji wake pindi zinapohitajika na watumiaji, huku nakala halisi zikilindwa katika kuziwezesha kudumu muda mrefu.

Vilevile, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inashughulika na usimamizi, ukusanyaji na uhifadhi wa kumbukumbu na vitu vya waasisi wa taifa, ambao ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, vyenye umuhimu wa kihistoria kitaifa.

Ukosefu wa kumbukumbu na nyaraka, inaelezwa kutoa mianya ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, matumizi mabaya ya madaraka na hata kuchelewesha au kuzuia haki kutendeka.



Kazi ya uhifadhi wa Nyaraka kwenye Mifumo ya kielektroniki kwa kutumia vifaa vya kisasa ili kutunza na kulinda historia andishi kitaifa. **PICHA ZOTE: MARY MWAKAPENDA**

> **Hadi sasa Idara ya Masijala imekwishakamilisha ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu cha Kanda ya Ziwa – Mwanza, ikiwa na uwezo wa kuhifadhi takribani jumla ya majalada 117,600 yaliyoko kwenye mfumo wa karatasi.**



Mashubaka ya kuhifadhi Kumbukumbu na Nyaraka katika Makao Makuu ya Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka zaTaifa, jijini Dodoma.



Rais Samia Suluhu Hassan

### HALI YA KUMBUKUMBU

Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa katika kipindi cha mwaka mmoja wa serikali iliyoko imefanikiwa kukusanya majalada muhimu 6,413 katika historia ya nchi, kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya 23, mamlaka za Serikali za mitaa 19 na taasisi za umma mbili.

Ili kuzisaidia taasisi za umma kuondokana na mrundikano wa kumbukumbu ambazo muda wa matumizi yake umekwisha na kutunza zile zenye umuhimu wa kudumu (urithi andishi) kwa ajili ya kusaidia rejea, tafiti na kutunza historia ya nchi, idara imeratibu na kusimamia ukamilishaji miongozo ya hifadhi na kuteketeza kumbukumbu kisheria. Hadi sasa jumla ya taasisi za umma nne zimeshatengeneza miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu.

Utunzaji sahihi wa kumbukumbu unachangia huduma bora kwa wananchi, kuimarisha utawala bora na uwajibikaji serikalini. Hivyo, katika kufikia lengo hilo katika kipindi cha mwaka mmoja ujao, serikali imeiwezesha Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa kufanya mikutano kazi 14 na mafunzo kwa wadau wa menejimenti, waratibu na watunza kumbukumbu.

Maeneo mengine ni kwenye taasisi za umma ikigusa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utunzaji taarifa, kumbukumbu na nyaraka za serikali, ili kuwajengea uwezo watumishi hao katika utumiaji na utunzaji wa kumbukumbu wanapotekeleza majukumu yao.

### HATUA ZA MABORESHO

Kwingineko kunajumuisha sasa serikali inapojielekeza na kujinufaisha katika kuwaenzi waasisi wa taifa letu; Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume.

Hapo, idara hiyo imeweza kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbuku na vitu vya waasisi hao wa taifa kutoka katika taasisi za umma na watu binafsi.

Katika mwaka mmoja uliopita, idara hiyo imekusanya jumla ya kumbukumbu 821 za waasisi wa taifa, ambazo ni vielelezo vya fikra na falsafa zao kwa ajili ya matumizi ya vizazi vya sasa na vijavyo katika kujiletea maendeleo na serikali imekuwa ikisisitiza kila mara katika utunzaji wa siri za serikali kwa viongozi na watumishi katika taasisi za umma.

Akizungumza na mawaziri, pia manaibu wao mnamo Januari 13 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, anasema mara kadhaa kumeonekana baadhi ya nyaraka za serikali zikitumwa na kujadiliwa katika mitandao ya kijamii, kitu ambacho ni kinyume na taratibu.

Hivyo, Rais anawaelekeza viongozi na watumishi wa umma kurekebisha kasoro hizo, kwa lengo la kuziba mianya inayotumika kutoa taarifa za siri za serikali.

Katika utekelezaji agizo hilo, idara husika ya kumbukumbu, imefanya tathmini na ufuatiliaji mifumo ya utunzaji kumbukumbu katika taasisi za umma 152, lengo ni kufahamu undani na hali halisi ya utunzaji kumbukumbu za serikali, ili kubaini kasoro zilizopo kwa ajili ya kufanyiwa maboresho kwa mifumo na kutoa elimu ya utunzaji kumbukumbu.

Idara hiyo ya Masijala, imepiga hatua katika kusogeza huduma za kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka, kutoka taasisi za umma zilizopo Kanda ya Ziwa.

Hadi sasa Idara ya Masijala imekwishakamilisha ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu cha Kanda ya Ziwa - Mwanza, ikiwa na uwezo wa kuhifadhi takribani jumla ya majalada 117,600 yaliyoko kwenye mfumo wa karatasi.

Rai inayowekezwa wakati wote, kutokana na umuhimu wa utunzaji kumbukumbu, ni vyema taratibu za utunzaji wa kumbukumbu ukazingatiwa katika taasisi za umma ili kupatikana huduma bora kwa maendeleo ya taifa.

***• Mwandishi wa makala hii ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Ofisi ya Rais; Utumishi.***

## TAFAKURI YA MLALAHOI




# Hili la Russia vs Ukraine linatufunza nini masikini?



**NA JOSEPH KULANGWA**
**+255 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

TUKIWA bado wadogo, tukiishi na wazazi wetu, tulizoea kumwona baba kila siku za Jumapili jioni akitoka nyumbani akimuaga mama anakwenda kwenye kikao cha mtaa.

Na kila akirejea alimsimulia mama nini kilijiri na mijadala ilihusu nini, lakini tukawa tukisikia kuwa ilihusu usalama wa mtaa na mipango ya maendeleo mtaani kwetu.

Lakini, wakati huo tukijua kuwa katika mtaa ule, kulikuwa na familia iliyokuwa ikijiweza kidogo ikilinganishwa na familia zetu, lakini ilikuwa na mtoto wao ambaye tulizoea kumwita Jabali.

Mtoto huyo wa kiume, alikuwa mkubwa kwetu na hakuwa anasema kama sisi, pia kila siku aliondoka nyumbani na baiskeli yake ya kifahari hivi akizunguka mitaani na kutamba.

Pamoja na kufanya ubabe huo, lakini hata siku moja hatukusikia amеadhibiwa, kwani ilikuwa kawaida yake kama si kutupora vitu vidogo vidogo ikiwamo mipira ya soka, alitukong'ota makonzi kila alipojisikia.

Mbaya zaidi alikuwa akivuta sigara na pengine hata bangi, kwani nyakati hizo alikuwa akitutuma madukani kumnunulia sigara, lakini siku ambazo hakututuma tulimwona akivuta sigara aliyosokota mwenyewe. Tulipoendelea kutambua mambo tukaja kugundua kuwa kumbe hata bangi alikuwa akivuta. Hatukusikia hata siku moja kapigwa na wazazi, kajadiliwa kwenye kikao cha kina baba au hata polisi tu.

Pamoja na udogo wetu, tukawa tunashindwa kuwaelewa wazazi wetu, kwamba kwanini hawakuwa wanaliona tatizo hilo mtaani kwetu na kuchukua hatua ya kutunusuru sisi kuonewa na jabali hilo?

Hatimaye, tukawa tunajiaminisha kuwa pengine umasikini wetu ndio uliofanya hata wazazi wasimwambie mzazi mwenzao tajiri kumkemea kama si kumchukulia hatua mwanawe. Tukahisi pengine wazazi wetu, kuna kitu walikuwa wananufaika kwa jirani yao huyo aliyemiliki duka, na magari kadhaa hivi. Hivyo, wakimwogopa kumkemea sembuse kumshitaki mtoto wake!

Yawezekana utajiri wake pia aliupata kwa njia haramu za dhulmat au hata ujambazi na njia zingine za aina hiyo, zisizokubalika hata kwa Mwenyezi Mungu.

Nimekumbuka haya kutokana na hiki kinachoendelea kwa wenzetu wa Ukraine, ambao wanavurumishiwa makombora kila kukicha, yakiua na kuharibu majengo na miundombinu. Ukraine hivi sasa wanachachafywa na Russia kila kona, wananchi wake wanapoteza maisha na wengine wanakimbia. Wageni wakazi wa nchi hiyo nao wanatafuta pa kutokea na wanaofanikiwa wanaondoka.

Hamkani si shwari tena katika taifa hilo, ambalo lilijitenga kutoka kwa Mrusi, ambaye kumbe hataki likajiunge na Umoja wa Kujihami wa Mataifa ya Ulaya (NATO) pia Umoja wa Ulaya (EU).

Jabali Russia anaingia Ukraine anavyotaka na kufanya mauaji na uharibifu kwa kiwango cha juu. Ukraine na Rais wake wanapiga makelele ya kuomba msaada, huku na kule duniani, lakini inaonekana kama sauti inagonga mwamba.

Marekani wanapiga kelele wakiwa chumbani kama ambavyo sisi vijitaifa vidogo tunavyopiga makelele sawa na ule usemi wa Kifaransa kuwa 'Le chien abois la caravane passe!" Yaani, kubweka kwa mbwa hakuzuii lori kupita.

Unajiuliza sasa hivi inakuwaje, hata mataifa makubwa yanayoweza kuvimbishiana vifua na Russia nayo yanaonekana kuingia uvunguni na kukiacha kitaifa hiki cha Ukraine, kikijililia chenyewe?

Kuna vyombo vya kimataifa kama Umoja wa Mataifa (UN), mbona nayo iko pembeni inapiga ukelele, tu huku moja ya mataifa yake likinyanyaswa na Taifa lingine? Huu ni sawa kabisa na jinsi tulivyokuwa tukiishi na familia ya Jabali mtaani. Tukitazama ulimwengu unavyokwenda, tunapata ukakasi kuona hata nyimbo kama Umoja wa Afrika (AU) yanapotokea matatizo katika baadhi ya mataifa, hatuoni ukijikusanya kukabiliana nayo.

Tunaona kinachoendelea Cabo Delgado, Msumbiji ambako magaidi wa Taifa la Kiislamu (IS) wameweka makazi na kushambulia taifa hilo masikini kama sisi tu. Hivi AU haijaliona hilo ikaingia kusambatarisha huko?

Je, jabali Russia anatupeleka wapi sisi walimwengu? Je tuendelee kumtazama tu akiharibu maisha ya binadamu wenzetu na kutafuta kuifuta Ukraine? Kama Vladmir Putin hataki mazungumzo, anataka nini? UN, AU, NATO na EU? Bila shaka wana majawabu. Alamsiki!

MTAALAMU UCHUMI:

# Staili ya uchumi wa Rais Samia, ina nuru leo, matarajio kesho

• Anaona uhai wa diplomasia uchumi • Fedha zinasogea mkononi mwa mtu • Staili yake kuwa msikivu 'inalipa'

**Na Sabato Kasika**

JANA umma wa Watanzania wakiongozwa na Rais wa sasa, Samia Suluhu Hassan, walikuwa mjini Chato kwenye tukio la maombolezo na kumbukizi ya mwaka mmoja kukamilika tangu kifo cha Rais Dk. John Magufuli, umma ulikusayika mjini Chato, katika tukio la kumbukizi ya mwaka huo mmoja wa kifo chake.

Pia, kesho unatimu mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia. Naam! Kumekuwapo mijadala kutoka kwa watu wa kada mbalimbali, wakitathmini utendaji wake na alikoifikisha nchi tangu aliposhika nafasi hiyo.

Nipashe ikaamua kuzungumza na mtaalamu wa uchumi na mshauri wa mambo ya fedha, Marko Sillayo, anayefanya shughuli zake binafsi jijini Dar es Salaam, ambaye anaanika mengi yanayokua kiuchumi katika mwaka huo mmoja wa kiutawala.

Silayo anafafanua kuwa mafanikio ya kiuchumi yanaonekana kibiashara kwa mtu mmoja mmoja au kiujumla katika nchi na kwamba, huenda ikawa si rahisi kuelezea mafanikio ndani ya kipindi kifupi cha mwaka mmoja, ila anataja dira na mwelekeo wa nchi kuimarika kiuchuni unatia matumaini.


"Kama unakumbuka kulikuwapo miradi mingi mikubwa aliiacha Rais Dk. John Magufuli na mingi imekuwa ikiendelezwa na mingine mipya kuanzishwa. Ni kipindi kifupi kwa kiongozi yeyote kuweza kuleta mageuzi ila hatua za awali zinaonyesha uelekeo si mbaya," anasema Sillayo.

Mtaalamu huyo anasema, pamoja na wimbi la corona kutikisa, Rais Samia ameweza kuleta matumaini makubwa kwa kuwa kwenye sekta ya uwekezaji, viwanda vipya vingi vinaendelea kuanzishwa.

"Mama (Rais Samia ) amekuwa mstari wa mbele kufungua milango kwa mataifa makubwa kuja kuwekeza nchini. Hii inaleta matumaini makubwa kwa nchi, japo ina gharama zake ila inaonyesha nuru ya tuendako," anafafanua.

Anakieleza kitendo cha kuvunja ukimya na kuamua kufunga safari kwenda kutia saini mikataba ya miradi mkubwa, ni ishara ya mafanikio katika uchumi nchini ndani ya uongozi wake ndani ya mwaka mmoja.

Mbali na hayo, anataja misamaha au punguzo la kodi kwenye miradi mikubwa na ya muda mrefu kuwa ni kitu ambacho kimeshaanza au kipo mbioni, kuanza na kwamba kitafungua milango mingi zaidi ya uwekezaji.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa katika picha ya pamoja na Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel, mara baada ya kuwasili katika makao makuu ya baraza hilo, jijini Brussels, Ubelgiji tarehe 15, mwezi uliopita. **PICHA: IKULU**

> **"Yapo mambo yanayozingatiwa yakijumuisha kuvutia wawekezaji, kukuza biashara na kuimarisha ushirikiano, pia utendaji wa mabalozi wa Tanzania unapimwa jinsi wanavyotekeleza dhana hii.**

### ANAFANANA NA WENZAKE

Mtaalamu Sillayo anasema, tangu Rais aingie madarakani ameshafanya mikutano kwa njia ya mtandao, kusafiri katika nchi mbalimbali na kuzungumza na viongozi wengi wa taasisi za kimataifa kwenye maeneo ya uchumi, uhusiano kimataifa, fedha huku akitembelea nchi mbalimbali.

"Kwa nchi maskini kama Tanzania, njia pekee ya kupiga hatua ni kutumia diplomasia vizuri katika uhusiano na taasisi na nchi nyingine. Rais aliwahi kutumia msemo kwamba 'Kama unataka kwenda haraka, tembea peke yako. Kama unataka kwenda mbali, nenda na wenzako'..." anasema Sillayo.

Katika ufafanuzi wake mtaalamu huyo wa uchumi anafafanua maana ya usemi huo wa Rais, kwamba ili Tanzania ipige hatua mbalimbali za kimaendeleo, ni muhimu ikashirikiana na nchi nyinginezo na siyo kujitenga.

Sillayo anafafanua kwa kina maeneo ambayo Rais Samia ameshatembelea ni nchi nyingi za Afrika, Ulaya na Amerika na kwamba, pia ameshahutubia Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, kikao ambacho kina hadhi kubwa sana kimataifa.

Anasema, kwa sasa dunia inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo janga la maradhi ya corona, namna bora zaidi ya kukabiliana nao, ni kwa ushirikiano kupitia nchi za jumuia za kimataifa.

### DIPLOMASIA YA UCHUMI

Rais Samia anasema hadi sasa diplomasia ya uchumi ni dhana inayojiegemeza kwenye uwekezaji na biashara na Rais anautilia mkazo, huku wanadiplomasia wa Tanzania nje ya nchi wakitegemewa kukuzwa kwa diplomasia hiyo.

"Yapo mambo yanayozingatiwa yakijumuisha kuvutia wawekezaji, kukuza biashara na kuimarisha ushirikiano, pia utendaji wa mabalozi wa Tanzania unapimwa jinsi wanavyotekeleza dhana hii," anasema.

Lingine, anataja baadhi ya mambo yanayopaswea kuzingatiwa kwenye diplomasia ya uchumi ni kuvutia uwekezaji kutoka nchi nyingine, huku ujuzi maalumu ukipewa umuhimu, kama vile kuwa na namna ya kujua fursa za uwekezaji zilizopo nchini.

"Fursa hizo zinaambatana na miradi inayoweza kutekelezwa, lakini fursa na miradi hiyo inapaswa kubainishwa katika mikoa na wilaya zote na maeneo ya kipaumbele," anasema.

Lingine, mchumi Sillayo ana hoja kwamba, dhana nzima ya diplomasia uchumi inahusika na biashara na mambo ya kipaumbele kuwezesha biashara na nchi za nje, ili ifanyike kwa urahisi, ikiwamo kununua na kuuza bidhaa na huduma kati ya nchi husika na mustakabali mpana kwa uchumi wa nchi.

"Ni muhimu kujua wawekezaji wanataka nini kabla hawajafanya uamuzi ili kurahisisha juhudi za kuwavutia, na ukiangalia ziara za Rais zimekuwa zikijikita katika hayo ili wawekezaji wanapokuja, kuwe na mkakati wa kuhakikisha wanaendelea kuwepo nchini," anasema.

### MAKALI YANAPUNGUA

Sillayo anasema, kwa sasa upatikanaji tenda za kazi kwa wafanyabiashara wadogo umeibuka na anaamini kuwapo kwake kunaweza kuwa kipimo cha mafanikio kwa watu wenye maisha ya kawaida, jambo linaloonekana kwa kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani.

"Ukweli ni kwamba 'vijitenda' (kandarasi) vimekua vinapatikana, tofauti na miaka ya nyuma. Pia, misamaha au punguzo la kodi kwenye miradi mikubwa na ya muda mrefu, ni jambo ambalo limeshaanza kutekelezwa au lipo mbioni kuanza... kutafungua milango mingi zaidi ya uwekezaji," anasema.

Kwa mujibu wa Sillayo,licha ya kuwapo vilio vya kukosekana fedha za kutosha mikononi mwa umma, lakini maoni yake ni kwamba, mwendo wa kiuchumi ulioko sasa, kuna dira ya kwamba uchumi utaimarika zaidi.

"Pamoja na hayo, nina ombi kwa Rais kwamba, aendelee kutana na wadau wengi wakiwamo wa upinzani kuweka mambo mezani na kuruhusu mijadala iendelee ili kuiendeleza nchi. Hili ni kubwa kuliko yote kwani ndiko maoni, ushauri vinakotoka," anasema.

Anamtetea Rais Samia, kwamba ni mtu wa kupokea mawazo kutoka pande mbalimbali na baadhi ameyafanyia kazi papo kwa hapo, huku mengine anayatolea ahadi kuyafanyia kazi, ikiwa inaleta matumaini kwa wananchi na kuweka mazingira mazuri ya ujenzi wa taifa.





## Tiba mbadala yaikosha serikali vita vya corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeitaja tiba asili na mbadala kuwa moja ya sababu iliyochangia kuiondolea mzigo serikali ya kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa virusi vya corona kwenye mlipuko wa kwanza mwaka 2020.

Kutokana na hali hiyo, imeahidi kuandaa mashamba ya miti tiba kila kanda nchini ambayo yatatumika kutoa dawa za kutibu magonjwa mbalimbali.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa UVIKO-19 na tishio la mlipuko wa kirusi kipya.

Alisema katika mlipuko wa kwanza wa UVIKO-19 nchini hali ilikuwa mbaya lakini njia zilizotumika zilisadia kupunguza idadi ya wagonjwa.

"Ugonjwa huu ulipoingia hali ilikuwa mbaya sana lakini tunashukuru hatua tulizochukua kama taifa ikiwemo matumizi ya tiba asili zilituokoa sana katika mapambano dhidi ya UVIKO-19."

"Matumizi ya tiba asili yalisaidia kuboresha afya za wananchi wetu na yalitubeba sana bila tiba asili hali ingekuwa mbaya sana maana tulikuwa tunaambiwa tungekuwa na wagonjwa hadi 50,000 kwa siku lakini hali hiyo haikufika kutokana na matumizi ya tiba asili,"alisema Ummy.

Alisema kutokana na tishio hilo serikali iliandaa uwanja wa saba saba kwa ajili ya kupokea idadi kubwa ya wagonjwa iliyokuwa ikitarajiwa.

"Lakini kutokana na tiba asili hali hii hatukuweza kuifikia kama ambavyo mataifa ya wenzetu walivyopata shida ya mlundikano wa wagonjwa pamoja na vifo vingi,"alisema.

Kadhalika, alisema hatua nyingine ambazo zilisaidia nchi kupunguza taharuki ni uamuzi wa kutowafungia ndani wananchi.

"Kama kuna kitu ambacho kilitusaidia ni kutoweka 'lock down' kama mataifa ya wenzetu hali hii ilisadia kulinda uchumi wa mtu mmoja na taifa kwa ujumla, hali zetu tunazifahamu kama tungefungia watu ndani hali ingekuwa ngumu sana"alisema

Vilevile, alisema hatua nyingine ni kuwaondolea hofu wananchi na kuwajengea imani kuwa UVIKO-19 ni ugonjwa kama ilivyo magonjwa mengine.

"Hii ndiyo maana unaona leo pia mataifa mengine yameachana na utaratibu wa kufungia watu ndani na kama mnavyoona hadi leo hii ugonjwa bado upo hivyo inabidi kuendelea kuishi nao na shughuli nyingine kuendelea kama kawaida,"alisisitiza Ummy.

# Bilioni 139.8/- zalipa maslahi ya watumishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetumia zaidi ya Sh.bilioni 139.81 ndani ya mwaka mmoja kwa ajili ya kulipa maslahi ya watumishi wa umma ikiwamo upandishaji vyeo na mishahara.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mafanikio yaliyopatikana ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema watumishi 190,781 wenye sifa stahiki wamepandishwa vyeo na madaraja huku Sh.bilioni 91.08 zikitumika kulipa madeni ya mishahara ya Watumishi wa Umma 65,394. "Kuwabadilisha kada Watumishi wa Umma 19,386 na kuwalipa mishahara mipya yenye thamani ya Sh.bilioni 1.33, kutoa vibali 12,336 vya ajira mpya na mbadala ambapo Sh.bilioni 7.76 zimelipwa na pia tumewapunguzia kodi watumishi wa umma kutoka asilimia tisa mpaka nane,"alisema.

Kadhalika, alisema katika kipindi hiko cha mwaka mmoja, Ofisi hiyo imefanikiwa kuanza kujenga Mfumo mpya wa Usimamizi wa Utendaji Kazi kwa Watumishi wa Umma (PEPMIS) ili kuondokana na kero za usimamizi wa utendaji kazi zilizojitokeza katika utekelezaji wa mfumo wa awali wa OPRAS.

"Mfumo wa OPRAS haukuakisi hali halisi ya utendaji kazi wa watumishi hali iliyoleta hisia za kupendeleana au kuoneana na kutokutumika kwa matokeo ya utendaji kazi katika kufanya maamuzi ya kiutumishi,"alisema.

Akizungumzia uhuishaji wa Sera, Kanuni za Utumishi wa Umma na Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Mhagama alisema Ofisi hiyo imeanza kufanya tathmini ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2008 kwa lengo la kuihuisha ili kuendana na mahitaji na mazingira ya sasa katika usimamizi wa utawala na utumishi wa umma.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (katikati), akipata maelezo kutoka kwa mjasiriamali, alipotembelea maonyesho ya wajasiriamali katika viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake watakiwa kuitumia fursa ya ardhi

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Jinsia na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wanawake kuchangamkia fursa zilizopo za ardhi kujikwamua kiuchumi.

Dk. Gwajima alitoa ushauri huo wakati akifungua mkutano wa 66 wa kimataifa wa kuangalia kamisheni ya hali ya wanawake hususani katika masuala ya umiliki wa ardhi(CSW 66),uliofanyika kwa njia ya mtandao akiwa nchini Marekani.

Mkutano huo umeratibiwa na Shirika lisilo la kiserikali la Landesa, Oxfam kwa kushirikiana na serikali.

Alisema serikali imekuwa ikihamasisha wanawake wasibaki nyuma na badala yake wajiinue kiuchumi kutokana na fursa zitokanazo na ardhi.

"Serikali iko makini kuhakikisha usawa unakuwepo kwa wanawake kushirikishwa katika kutoa maamuzi kwenye masuala ya ardhi vijijini na mijini ili kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma,"alisema.

Alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa wanawake vijijini na mijini ya kuwafanya kutambua haki yao ya ushirikishwaji wa utoaji maamuzi katika masuala muhimu ya ardhi na haki nyingine za msingi.

"Sote tunaamini kwamba wanawake hawawezi kutenganishwa na ardhi endapo ardhi imepangwa kuwa kitega uchumi kwa jamii kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi," alisema Dk. Gwajima.

Awali, Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Prof. Gaston Kenned, alisema mkutano huo ni muhimu na ni nafasi nzuri kwa Tanzania kuwasilisha ajenda zao ambazo zitasikilizwa na kujadiliwa.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi kutoka Wizara hiyo, Rennie Gondwe alisema huwa wanashiriki mkutano kama huo kila mwaka kwa ajili ya kujua kamisheni ya hali ya wanawake duniani hususani katika suala zima la umiliki wa ardhi.

Alisema mwaka huu mkutano huo umefanyika nchini Marekani na Waziri Gwajima amewakilisha huku wao kama wadau wa maendeleo wameshiriki kwa njia ya mtandao nchini.

"Tunafurahi hivi sasa wanawake wengi wanashirikishwa katika masuala ya umiliki wa ardhi na hii inatokana na sheria kubadilika ambayo inaondoa suala la mfumo dume na kuwa mwanamke hapaswi kumiliki ardhi,"alisema Gondwe.

Gondwe alisema wadau wa maendeleo ya jamii wamekuwa wakisaidia kuelimisha jamii kuhusu haki za wanawake katika kumiliki na kushirikishwa kwenye utoaji wa maamuzi.

Kwa upande wake, Dk. Monica Mhoja ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Landesa Tanzania, alisema kumekuwapo na mila na desturi potofu na zinazomkandamiza mwanamke hivyo wadau wa maendeleo wamekuwa wakisaidia kupiga vita mifumo dume kwa jamii.

Alisema Shirika hilo limejikita katika kuangalia masuala ya ardhi na usalama wa ardhi hususani kwa wanawake wanaoishi vijijini na wamekuwa wakitoa elimu ya ushirikishwaji wa maamuzi kwenye masuala ya ardhi.

Alisema baadhi ya makabila kumekuwa na mifumo dume ambayo inawakandamiza wanawake jambo ambalo sio sahihi.





# Mbeya-WSSA kupanda miti 1,500

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), inakusudia kupanda miti 1,500 kwenye vyanzo vitatu vya maji ndani ya wiki moja ili kuvilinda visikauke pamoja na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

Aidha, mamlaka hiyo inakusudia kutoa elimu ya mazingira na upandaji wa miti kwa wananchi wa mkoa huo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Maji Duniani.

Kaimu Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Simon Bukuku, alibainisha mpango huo juzi wakati wa uzinduzi wa zoezi la upandaji wa miti katika chanzo cha maji cha Mwashali kilichoko katika Kata ya Isyesye jijini Mbeya ambako wafanyakazi wa mamlaka hiyo na wadau wengine walipanda miti 500.

Alisema mbali na chanzo hicho pia watapanda miti katika chanzo cha maji cha Ilunga kilichoko Kata ya Utengule - Usongwe na chanzo cha maji cha Itangano ambacho kipo Uyole na kwamba katika kila chanzo watapanda miti 500.

Bukuku alisema miti wanayopanda ni ile ambayo ni rafiki kwenye vyanzo vya maji, huku akidai kuwa mbali na miti hiyo pia watawahimiza wananchi kupanda miti kwenye maeneo yao ili kutunza mazingira.

"Tutatoa pia elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji hasa kwa kuwahimiza kupanda miti, mbali na hiyo pia tutafanya mambo mengine ya kijamii ikiwamo kurejesha sehemu ya mapato tunayopata kwa kuwasaidia wahitaji," alisema Bukuku.

Alisema katika kipindi hiki cha maadhimisho ya Wiki ya Maji, mamlaka hiyo imetoa ofa maalumu kwa wananchi ambao walisitishiwa huduma ya maji kutokana na kutolipia huduma hiyo kwa kuwaruhusu walipe nusu ya fedha walizokuwa wanadaiwa ili warejeshewe huduma.

Akizindua zoezi la upandaji wa miti kwenye vyanzo vya maji, Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Mbeya-WSSA, Edna Mwaigomole, aliwataka wadau kushiriki katika utunzaji wa vyanzo vya maji ili huduma hiyo iwe endelevu.

Alisema mbali na upandaji huo wa miti, pia wanatakiwa kuitunza ili isikauke na kwamba wanatakiwa wawe wanafanya tathmini kila mwaka ili kujua kama miti wanayopanda inaendelea vizuri.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo pia kupanda miti kwenye makazi yao ikiwamo ya matunda, kuni na kwamba kwenye vyanzo vya maji kuna miti maalumu inayostahili kutumika kwenye vyanzo vya maji.

"Tupande miti kwenye maeneo yote ya vyanzo vya maji, pembezoni mwa mito na kwenye maeneo yenye ardhioevu, lakini tupande miti ya matunda ili itusaidie sisi na vizazi vyetu," alisema Mwaigomole.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji Mijini na Vijijini, Emile Mpasi aliwataka wananchi kuhakikisha wanalipia huduma za maji ili kufanikisha utekelezaji wa miradi mingine ya maji.

Vilevile aliwataka wananchi kutoa taarifa za upotevu wa maji ili wataalamu wa mamlaka wafike na kudhibiti upotevu huo akidai kuwa uzalishaji wa maji unatumia gharama kubwa.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), Edna Mwaigomole, akijiandaa kupanda mti katika chanzo cha maji cha Mwashali, Kata ya Isyesye, jijini Mbeya juzi, ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa Wiki ya Maji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Machinga Mbeya wamkumbuka JPM

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

WAFANYABIASHARA wadogo maarufu machinga katika Mkoa wa Mbeya wamesema wanamkumbuka aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli, wakidai kuwa aliwasaidia kufanya kazi zao kwa uhuru.

Dk. Magufuli alifariki dunia Machi 17, mwaka jana, wakati alipokuwa anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Mzena jijini Dar es Salaam ambapo kifo chake kilizua simanzi na majonzi miongoni mwa Watanzania.

Wakizungumza na Nipashe jana ikiwa ni mwaka mmoja tangu alipofariki Dk. Magufuli, machinga wa Jiji la Mbeya walisema utaratibu wake wa kuwaruhusu kufanya biashara mahali popote bila kutozwa ushuru uliwasaidia kuinuka kiuchumi.

Mmoja wa wamachinga hao, Timothy Mwalunyasi, alisema awali walikuwa wanafukuzwa kwenye maeneo waliyokuwa wakifanyia shughuli zao lakini, Dk. Magufuli alipotangaza kwamba wasisumbuliwe walikuwa huru.

Alisema Dk. Magufuli ndiye mwanzilishi wa vitambulisho vya machinga ambavyo vimekuwa vikiwasaidia kufanya shughuli zao bila kusumbuliwa na maofisa wa serikali hasa wanaokusanya mapato.

"Lakini kwa hapa Mbeya alitupatia eneo la Uwanja wa Ndege wa Zamani ili tulitumie kwa ajili ya biashara zetu na sasa hivi tunaendelea kuboreshewa miundombinu ili tufanye shughuli kwenye mazingira rafiki," alisema Mwalunyasi.

Ipyana Mbilinyi, mfanyabiashara wa viatu, alisema kwa mara ya kwanza machinga walianza kutambulika wakati Dk. Magufuli alipoingia madarakani kwa madai kuwa shughuli yao ilianza kuonekana kuwa ni kazi rasmi.

Alisema kabla ya hapo shughuli hiyo ilikuwa inaonekana kama ya wahuni, lakini Hayati Magufuli akaondoa hiyo hali na wao wakawa wanaonekana kama watu wanaofanya kazi rasmi.

"Tunashukuru mama yetu, Samia Suluhu Hassan naye ameendeleza utaratibu wa kututambua sisi na kazi yetu, tunaamini ataendelea nasisi mpaka atakapomaliza muda wake," alisema Mbilinyi.

Naye Nyoni Sumbuko alisema Dk. Magufuli mbali na kuwasaidia wao pia aliifanya Tanzania itambulike zaidi kimataifa kutokana na misimamo yake kwenye mambo mbalimbali ikiwamo mapambano dhidi ya mafisadi na uhujumu uchumi.

Alisema baada ya kifo cha Dk. Magufuli walikuwa na wasiwasi kwamba Rais Samia asingeweza kuiongoza vizuri nchi, lakini kwa mwaka mmoja ambao ameongoza wameanza kuwa na imani naye.Jana kumbukizi ya mwaka mmoja wa kifo cha Dk. Magufuli ilifanyika katika Wilaya ya Chato mkoani Geita ambapo Rais Samia Suluhu Hassan aliwaongoza Watanzania.

Dk. Magufuli alijizolea umaarufu duniani kutokana na usimamizi wa miradi na kupambana na mafisadi na wahujumu uchumi, lakini alijipatia umaarufu zaidi kwenye vita dhidi ya ugonjwa wa corona.

# Benki ya Exim yatoa msaada madawati 100

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya Exim Tanzania imeikabidhi Serikali ya Mkoa wa Mbeya msaada wa madawati 100 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 20 ili kusaidia kukabiliana na tatizo la upungufu wa samani hizo kwenye shule za serikali.

Makabidhiano ya msaada huo yalifanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na kuhudhuriwa na maofisa mbalimbali wa benki hiyo na wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu, alisema madawati hayo ni sehemu ya 1000 ambayo benki hiyo inaendelea kuyatoa kwa mikoa mbalimbali nchini ili kusaidia kuboresha sekta ya elimu.

Alisema msaada huo unatolewa kupitia mpango wa Benki hiyo wa uwajibikaji kwa jamii (CRS) ujulikanao kama Exim Cares na kwamba kwa mwaka huu mpango huo unalenga kusaidia kwenye uboreshaji wa sekta ya elimu.

"Mpango huu ni wa nchi nzima ambapo mbali na mkoa wa Mbeya pia tunaendelea kukabidhi madawati haya katika mikoa yote nchini, lengo letu ni kufikisha madawati 1000 nchi nzima," alisema Kafu.

Alisema msaada huo ni sehemu ya ahadi ambazo benki hiyo ilimwahidi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa uzinduzi wa mpango huo mkoani Mtwara mwishoni mwa mwaka jana.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mkuu wa Mkoa, Juma Homera aliishukuru Benki ya Exim kwa msaada huo ambapo alisema msaada huo unakwenda sambamba na jitihada za serikali za kuboresha sekta ya elimu mkoani humo.

Alisema msaada huo utasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa madawati katika mkoa huo unaotokana na ongezeko la miradi mingi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa inayoendelea mkoani humo kwa sasa.

"Msaada huu utasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa madawati katika baadhi ya shule zetu, tunashukuru sana wenzetu wa Benki ya Exim kwa msaada huu na tunaomba mwendelee kusaidia kwenye maeneo mengine ikiwamo sekta ya afya," alisema Homera.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan anapambana kutafuta fedha kwa ajili ya miradi mikubwa inayoendelea nchini hivyo ni jambo linalotia moyo kwake kuona wadau kama benki wakiendelea kumuunga mkono.

Katibu Tawala wa Mkoa Mbeya, Angelina Lutambi, alizitaja baadhi ya shule zitakazonufaika na msaada huo kuwa ni Shule ya Msingi Mwenge na Shule ya Msingi Jitegemee za jijini humo zinazokabiliwa na uhaba mkubwa wa madawati.





## Mwakilishi ashauri wanawake kuwania nafasi za uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Baraza la Wawakilishi, Mwanaasha Khamis Juma, amewataka wanawake kujitokeza kuwania nafasi za juu za uongozi kwa sababu mfumo dume umeanza kuondoka, ikiwamo wapigakura kuwakubali wanawake.

Alitoa ushauri huo katika kongamano kuhusu Siku ya Wanawake Duniani lililofanyika juzi Mjini Unguja ambalo liliandaliwa kwa pamoja na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA).

Alisema ni wakati wa wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi kutokana na jamii yenyewe kubadilika na kuona juhudi zinazochukuliwa na wanawake kwa wale waliopata nafasi ya kuongoza katika majimbo ya uchaguzi.

Alitoa mfano kwamba mwaka 2015-2020 alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Chukwani wa kuchaguliwa na wananchi na kuongoza kwa miaka mitano, lakini wakati akijitayarisha kugombea tena alijikuta Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ikifanya marekebisho makubwa ya mgawanyo wa majimbo na kulifuta jimbo hilo na kuanzisha Jimbo la Kiembesamaki.

Alisema mabadiliko hayo yalimchanganya kwa sababu jimbo ambalo amewekeza kwa kipindi cha miaka mitano halipo tena, hivyo analazimika kutafuta jimbo jingine hali, ambayo ilimlazimu kuanza upya harakati za siasa.

"Nilibabaika kidogo, lakini sikukata tamaa...niliamua kujitosa katika jimbo jingine la Dimani Mkoa wa Mjini Magharibi kwa nafasi ya uwakilishi na kupambana na zaidi ya wagombea 11 wanaume na kufanikiwa kuibuka na ushindi," alisema. Aliwataka wanasiasa wanawake wasiogope kugombea katika majimbo ya uchaguzi na kupambana na wanaume, ambapo uzoefu unaonyesha wanawake wameanza kukubalika kutokana na uaminifu wao na utiifu katika kuwatumia wapigakura.

Aliyekuwa mgombea wa nafasi ya ubunge Jimbo la Malindi, Halima Ibrahim kutoka Chama cha ACT-Wazalendo aliwataka wanawake kuungana na kuweka pembeni tofauti za vyama ili majimbo ya uchaguzi yanashikiliwa na wanawake.

Mwakilishi wa Viti Maalum, Salma Mussa Bilali, alisema yapo mabadiliko makubwa katika mwenendo wa siasa nchini ambapo wanawake wameanza kukubalika na kushika nafasi nyingi za uongozi na kuchaguliwa katika majimbo ya uchaguzi.

"Sina wasiwasi matarajio yangu makubwa kuona idadi ya wanawake katika majimbo ya uchaguzi itaongezeka kwa kiwango kikubwa katika uchaguzi mkuu ujao kwa sababu wanawake sasa wapo juu," alisema.

# Othman ahimiza jamii kufanya kazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema pamoja na changamoto nyingi zinazoikabili ustawi wa jamii nchini, katiba inasema ni wajibu wa kila mtu kujenga utamaduni wa kupenda kufanyakazi kwa moyo wa uzalendo na kuzingatia fursa ili kufanikisha maendeleo.

Othman aliyasema hayo katika maadhimisho ya Siku ya Ustawi wa Jamii, ambayo yalifanyika katika viwanja vya Kariakoo, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Alisema kuwa kifungu cha 10 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kinaeleza mambo muhimu ambayo inatakiwa kuyafuata ili kulinda na kuendeleza ustawi wa jamii, kwa madhumuni ya kujenga umoja, maendeleo ya watu na wajibu wa serikali katika kuchukua hatua kadhaa zilizoelezwa, ambazo ni kuhakikisha kwamba msaada unatolewa kwa wale wasiojiweza, wazee, wagonjwa, watoto na watu wenye ulemavu.

Aidha, Othman alieleza kwamba kipimo cha nchi au taifa lolote linalojali maendeleo ya kweli, ni pamoja na kuangalia mafanikio yake katika kujenga ustawi bora wa jamii, na wala si vinginevyo.

Hivyo alihamasisha haja ya kuitumia siku hiyo ya kimataifa ya ustawi wa jamii, kuhakikisha umma unapima na kuhamasisha wanaustawi kila mmoja kutekeleza wajibu wake kwa maslahi ya maendeleo ya Taifa.

Othman alieleza pia wajibu kwa vijana kupenda kujishughulisha na harakati mbalimbali halali za heshima na zinazostahiki, ili kuondokana na matatizo yatakayowapelekea kupoteza mwelekeo wa maisha yao ya baadaye, huku akitoa wito kwa maofisa, wazee, wanawake, watoto na wadau wote kushirikiana na kuunganisha nguvu za pamoja baina yao, jumuiya na taasisi zote katika kupambana na matatizo ya udhalilishaji.

"Nataka niwahakikishie kwamba serikali itaendelea kuwa mstari wa mbele kupinga udhalilishaji, mnaelewa kazi imeanza ikiwamo kuanzishwa kwa Mahakama Maalum ya kupambana na vitendo hivyo,"alisema.

Naye Waziri wa Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema kuwa maadhimisho hayo yanalenga katika kutambua na kutathmini juhudi za michango inayotolewa na maofisa na wadau wote wa ustawi jamii ili kufanikisha utoaji wa huduma, misaada na maendeleo.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni "kufanya kazi kwa pamoja, kutoa huduma bora za ustawi dhidi ya ukatili na udhalilishaji".



Baadhi ya vijana wakionyesha umahiri wao wa kuogolea kwenye Bahari ya Hindi, Forodhani, Mjini Unguja juzi.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Taasisi za huduma zatakiwa kumlinda mtumiaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amezitaka taasisi zinazohusika na kutoa huduma kuhakikisha zinashirikiana na majukwaa ya watumiaji katika kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ili kumlinda mtumiaji.

Hemed alitoa maelekezo hayo katika kilele cha maandimisho ya Wiki ya Mtumiaji yaliofanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar.

Alisema ni vyema kwa taasisi hizo kuzifanyia kazi kwa vitendo sheria na kanuni zilizopo ili kumsaidia mtumiaji kupata huduma bora bila viikwazo.

Alieleza kuwa wapo baadhi ya watumishi hawawajibiki ipasavyo na kusababisha wananchi kuumia kutokana na uzembe wa watumishi hao, hivyo aliwataka viongozi kusimamia sheria ili kufikia lengo la serikali kurahisisha huduma kwa wananchi wake.

Aidha, Makamu wa Pili wa Rais alizitaka mamlaka husika kuangalia njia bora za kiuendeshaji kwa lengo la kuwalinda watumiaji wa huduma mbalimbali.

Pia alizitaka taasisi hizo kuandaa malengo madhubuti ya kila mwaka kuwafikia wananchi kujua haki na wajibu wao na kusimamia kutoingizwa nchini bidhaa zisizokidhi vigezo ili kuwapunguzia wafanyabiashara wadogo kuingia katika hasara zinazoweza kuepukika.

Kwa upande wake Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduwara alieleza kuwa katika kujali na kuzingatia hali za wananchi wizara imeweza kushusha bei ya watumiaji wa umeme kwa asilimia 50 ili kurahisisha huduma kwa wananchi wa Zanzibar.

Kaduwara alieleza kuwa Baraza la Kuwawakilisha Watumiaji wa huduma za maji na nishati Zanzibar (CRC) wanaendelea kutoa elimu kupitia njia mbalimbali kwa wananchi ili watumiaji kujua haki na wajibu wao katika matumizi.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Watumiaji Tanzania, Leo Ngowi, alieleza kuwa jukwaa hilo humlinda mtoaji na mpokeaji katika kupata huduma kwa kuweka sera na sheria madhubuti ya kulinda haki hizo.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 30 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late**
**HARRIS CHRISTOPHER GARDIAS**
**By1. EVAN HARRIS GARDIAS.**
**2. ……………………………..**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 05day of April...2022
**Dated at Morogoro this 15 day of March..2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA PASIPOTI



**MANUEL ALEXANDER GOMES** anatangaza kupotea kwa pasipoti yake yenye namba za usajili **TAE125638** iliyotolewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia **PCO ZANZIBAR** iliyotolewa July 02 mwaka 2019
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. POLISI **TAARIFA:DSM/PHQ/RB/108825/2022**

**MIJNET COMPANY LIMITED**
**AUCTION MART MOROGORO**
**TANGAZO LA MNADA**

KWA NIABA YA NEEMA GROUP TUNAUZA DHAMANA YA GEORGE STEVEN MKANGA KAMA DHAMANA YA MKOPO ALIYOKOPA.DHAMANA YENYEWE NI KIWANJA PLOT NO 319 BLOCK Y MKUNDI KWA CHAULA MOROGORO.MNADA UTAFANYIKA TAREHE 19/03/2022.

SAA 5:00 ASUBUHI SIKU YA JUMAMOSI FIKA MAPEMA UKAKAGUE ENEO HUSIKA.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABUBAKAR MOHAMED YUSUPH**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya GARI (toyota hilux) ya bulldozer PLATE NUMBER **T 812 DRH** (CHASSIS NO: **AHTFR22GX06063631)/PLATE NUMBER T 433 DKC(CHASSIS CAT00D8RC9EM01951)** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba
**0677082401**
**MOR/MOR/RB/97499/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KILIFLORA C LIMITED**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya LANDROVER yenye USAJILI NAMBA **T605 AJC,** CHASSIS NAMBA **salldhac8aa238577.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/108943/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **BENJAMIN MAHUNDA RWAITAMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Isuzu lenye namba za usajili **T 578 DBS,** Injini namba **4JA1593214** na Chassis namba **NHR54C7112090,** linalomilikiwa na **RWAITAMA SPIRIT COMPANY LIMITED.**
Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/108670/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0754367365.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa wa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi na 11/2022**

**SIMONI ELIEZERI MGENI……………Marehemu**
**FURAHA JOSHUA MGENI…………..Mwombaji**

**ANGAZO KWA UMMA**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na Marehemu aliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya Mali za Marehemu na hesabu za mirathi katika katika jalada la mirathi. Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya Mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 10 ya mwezi wa April mwaka 2022.
**Imetolewa na Hakimu Mkazi leo siku ya tarehe 10 March mwaka 2022.**

Hakimu Mkazi

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GALEN GAUDANCE SILIVESTER** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 427 CTM – TVS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MSS/RB/12/2022.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 40 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PASCAL HERMENEGILD ISUJA OF MEMBE WARD CHAMWINO DISTRICT WITHIN DODOMA REGION.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY FLORA JOSEPH MAGORI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 28 Day of 4/2022.
Dated at Dodoma this 17 day of 3/ 2022.

**Presented for filling this 17 Day of 3/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA NA.36/2021**
**PROSPER EVARISTO SANGA……………..MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**SINA WILISON WALONDE……..MJIBU MAOMBI WA 01**
**JOB MWINUKA……………………MJIBU MAOMBI WA 02**
**CHRISTOPHER KINYUNYU……..MJIBU MAOMBI WA 03**
**YONO AUCTION MART & CO LTD..MJIBU MAOMBI WA 04**
**KWA: 1.CHRISTOPHER KINYUNYU**
**2.YONO AUCTION MART & CO LTD**
**POPOTE MLIPO---TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuliwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 24/03/2022 siku ya Alhamisi saa 3:00 asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA,ukikosa kufika mahakamani siku hiyo,shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolea.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 07 Machi,2022.

…………………………………
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DECAS BALTAZARY NYANZARA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **INDEX NAMBA S.1635/0034** kilichotolewa na Baraza La Mitihani La Taifa mwaka 2016 kupitia shule ya sekondari GWANUMPU . Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI **TAARIFA: KSD/RB/57/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAMES CRISTOPHER BROWN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye namba za usajili **T 602 DEU,** Engine No: **1CD0489660,** Chassis No: **JTEHG20VX00088475,**yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**TUN/RB/569/2022**

## KUPOTEA KADI YA GARI

HASSAN HASSAN ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI(ALFAD) yenye namba za usajili T784 DKH Chassis namba: ANH100048662
Injini namba : 2AZ1289826
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/98224/2022


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mkuranga yaanzisha programu afya shuleni

**Na Jenifer Gilla**

SHIRIKA la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), kwa kushirikiana na Wilaya ya Mkuranga, limeanzisha programu ya afya shuleni kwa kuzipatia shule vyumba vya huduma maalum za afya ili kuangalia hali za afya za wanafunzi wanapokuwa shuleni.

Ofisa Elimu wa Wilaya Sekondari, Benjamin Majoya, alisema jana kuwa takribani shule 22 kati ya 30 za sekondari za umma katika wilaya zinafanya programu hiyo inayotolewa na walimu wa afya waliohitimu mafunzo hayo.

"Wazo la asili la kuanzishwa kwa mfumo wa huduma za afya lilitoka lililetwa kwa mara ya kwanza na Azusa OSAWA ambaye alikuwa mtaalamu wa kujitolea kupitia Mpango wa Wataalamu wa Kujitolea kutoka Japan (JOCV) ambaye alihudumu hapa nchini kutoka 2011 hadi 2013," alisema.

Alisema mpango huo unasaidia wanafunzi hasa wa kike kufahamu hali zao za kiafya wanapokabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa ujana wao kwa huwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga inatoa huduma ya kwanza ikiwa ni pamoja na ushauri na elimu ya afya ya uzazi kwa vijana ili kufahamu mabadiliko ya kibaiolojia katika maisha yao na miili yao.

Kupitia programu hiyo, maofisa watatu wa Mkuranga walipata mafunzo nchini Japan kupitia mpango wa ushirikiano wa mafunzo ya JICA na kujiunga na kozi ya afya shuleni.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo, Halima Omary, mwalimu wa sayansi katika Shule ya Sekondari Kiparang'anda, alipongeza mpango huo akisema unalenga kuwawezesha wanafunzi kujua namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali katika ukuaji wao na hivyo kuweza kusimama kidete kufikia malengo yao ya kikazi ili kukamilisha masomo yao vizuri.

Programu hiyo ni zao la Mpango wa Ushirikiano katika Kukuza Maarifa wa JICA katika nchi ya tatu au mtandaoni.

Baadhi ya maarifa ambayo jamii ya kijapani imekusanya, ikiwa ni pamoja na uzoefu wake katika maeneo kama vile ujuzi wa shirika na mifumo ya kijamii, yanaweza kueleweka kwa ufanisi zaidi kupitia uzoefu wa kibinafsi. Mipango ni njia muhimu ya ushirikiano wa kiufundi ambayo inasaidia maendeleo ya rasilimali watu na kutatua masuala katika nchi zinazoendelea.

# MV Mwanza, Umoja mkombozi usafiri Victoria

**Na Waandishi Wetu**

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa meli ya MV Mwanza na ukarabati wa meli ya MV Umoja kutarahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji kwa mikoa inayozunguka mkoa wa Mwanza pamoja na nchi jirani zinazotumia Ziwa Victoria.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Mwanza na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, baada ya kukagua maendeleo ya ukarabati na ujenzi wa meli hizo huku akiahidi kuwa serikali itaendelea kutenga fedha ili kukamilisha miradi yote ya kampuni ya huduma za meli.

"Nipende kuwahakikishia kuwa kukamilika kwa ujenzi wa meli ya MV Mwanza kutatochea sana uchumi na kuongeza pato kwa mikoa inayozunguka Ziwa, lakini kukamilika kwa ukarabati wa MV Umoja kutarahisisha sana usafiri wa abiria na mizigo," alisema.

Naibu Waziri Mwakibete aliitaka Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuhakikisha inawasimamia kwa karibu makandarasi wote wawili wanaotekeleza mradi wa ujenzi na ukarabati ili wakamilishe miradi hiyo kwa kuzingatia thamani ya fedha, lakini kuongeza ujuzi kwa wataalamu wa ndani.

Aidha, Mwakibete alihakikishia MSCL kuwa changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo ikiwamo upungufu wa watumishi wa fani za uhandisi kuwa litashughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi ili kufanya taasisi hiyo iweze kuwa imara kiutendaji.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL, Philemon Bagambilana, alimhakikishia Naibu Waziri huyo kuwa taasisi imejipanga na inasimamia kwa karibu miradi hiyo ili kuleta matokeo ya uwekezaji unaofanywa na serikali katika ukanda huo.

Bagambilana aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwekeza kwenye taasisi hiyo na kusema moja ya matokeo ya uwekezaji kwenye ukarabati wa meli hasa za MV Victoria na MV Butiama ni kuongezeka kwa mapato kutoka Sh. bilioni moja kwa mwaka 2019 hadi kufikia Sh. bilioni 4.5 mwaka 2021.

Mradi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza unatekelezwa na Kampuni ya Gas Entec Company Limited na Kampuni ya KANGNAM Corporation kwa kushirikiana na SUMA JKT kwa gharama ya Sh. bilioni 96.9 na ukarabati wa meli ya MV Umoja unatekelezwa na SM Solution Co Ltd ya nchini Korea na unagharimu Sh. bilioni 19.




Mkurugenzi Mkuu wa TBL Plc, Jose Moran, akizungumza na wafanyakazi, wauzaji na wasambazaji wakuu wa bidhaa za kampuni hiyo, katika hafla ya uzinduzi wa huduma ya kununua bidhaa kwa njia rahisi ya programu ya mtandaoni ijulikanayo BEES, jijini Dar es Salaam jana. Huduma hii mpya inatumika katika nchi zaidi ya 20 na kutumiwa na wateja zaidi ya milioni 2. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati Bunge Mazingira ziarani Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira imefanya ziara Zanzibar na kukutana na kamati ya kusimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa wa Baraza la Wawakilishi.

Katika ziara hiyo iliyofanyika jana, kamati iliambatana na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, Naibu Katibu Mkuu (Mazingira), Edward Nyamanga na wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira, David Kihenzile, alisema ziara hiyo inalenga kukagua miradi ya mazingira inayotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kihenzile pia alisema wajumbe wa kamati yake wanakutana na kamati hiyo kwa lengo la kufahamiana na kujitambulisha kwa vile kamati hizo mbili zina majukumu ya kuisimamia serikali katika sekta ya mazingira.

Naibu Waziri Khamis alisema ziara ya kamati hiyo pamoja na wataalamu inalenga kukagua miradi ya kimazingira.

Khamis alisema suala la mazingira hususan katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi linagusa serikali zote mbili za Muungano na ile ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Alisema kutokana na changamoto hizo za kimazingira serikali hizi mbili zinafanya jitihada za dhati katika kukabiliana nazo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi, Mtumwa Pea Yussuf, alisema kamati yake inasimamia wizara nne ikiwamo Ofisi ya Makamu wa Rais (inayoratibu masuala ya mazingira), Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Tawala za Mikoa na Wizara ya Katiba na Sheria.

Alipongeza jitihada za serikali katika kushughulikia changamoto za kimazingira zinazoyakabili maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba zikiwamo ujenzi wa kuta za kupunguza mwimbi ya bahari katika ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi.

Mtumwa alitoa rai kwa serikali kuongeza kasi ya kutatua changamoto za mabadiliko ya tabianchi huku akionyesha wasiwasi wake kuhusu baadhi ya visiwa kuliwa na maji ya bahari na kupendekeza kamati hizi kutoka pande mbili za Muungano kushirikiana ili kunusuru mazingira.

# DUBE AFUNGA LA KWANZA, JULIO ASEMA WALIKAMIWA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI straika Mzimbawe wa Azam FC, Prince Dube akifunga bao lake la kwanza msimu huu, Kocha Msaidizi wa Namungo, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema timu yake ilikamiwa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi kwa wageni kupata ushindi wa magoli 2-1.

Dube alifunga bao la kusawazisha, likifuta lile la uongozi lililofungwa na Mohamed Banka wa Namungo, kabla ya Aziz Ismail kupachika bao la ushindi. Akizungumza na gazeti hili, Dube alisema bao hilo amelitoa zawadi kwa mashabiki wa Azam na wachezaji wenzake kwa sababu ni goli la kwanza huku binafsi akifurahi kwa sababu liliwapa faraja pia mashabiki wake.

"Nimefurahi kufunga bao langu la kwanza msimu huu, ilikuwa siyo rahisi, bao hili nalitoa kwa mashabiki waliosafiri kutoka kila sehemu kuja kutushangilia, pamoja na wachezaji wenzangu walinipa sapoti hadi kufanya hivi," alisema Dube ambaye msimu uliopita akishika nafasi ya tatu kwenye ufungaji bora.

Straika huyo alifunga mabao 14, akizidiwa mabao na mshindi wa kiatu cha dhahabu, John Bocco aliyekuwa na mabao 16 huku Chris Mugalu akiwa na mabao 15.

Kuhusu ufungaji bora, Dube alisema kwa sasa ni ngumu sana kufikiria kusaka kiatu cha dhahabu msimu huu baada ya kinara Fiston Mayele wa Yanga na Reliants Lusajo wa Namungo wenye mabao 10 kila mmoja wakizidi kufanya vyema.

Naye Julio alisema kipigo walichokipata kutoka kwa Azam FC, kilitokana na wachezaji wa timu hiyo kuipania zaidi mechi baada ya kupata matokeo mabaya michezo yao iliyotangulia.

"Azam ni timu nzuri, hiyo inaeleweka, lakini mechi hii wameonekana kupambana sana, wamejituma mno na walionekana wameipania na hii yote imetokana na kutokuwa na matokeo mazuri kwenye mechi zilizopita, kwa hiyo walicheza kwa nguvu zaidi kuliko sisi," alisema Julio.

Naye Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallim, alisema amefurahishwa na ushindi huo huku akiwapongeza vijana wake kwa kupambana, licha ya kutanguliwa bao la mapema.

Ni mechi ya kwanza kwa Azam kushinda tangu walipopata ushindi wa mabao 2-0 Februari 4, mwaka huu, dhidi ya Dodoma Jiji, lakini baada ya hapo ikachapwa magoli 2-0 na Biashara United halafu ikatoka suluhu na Coastal Union, kabla ya kufungwa bao 1-0 na Polisi Tanzania.

Kwa matokeo hayo ya juzi, Azam imepanda hadi nafasi ya tatu kwa kuwa na pointi 28, ikiiacha hapo Namungo yenye pointi 25, ikiwa kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.



Mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube (kulia), akiwania mpira dhidi ya winga wa Namungo, Shiza Kichuya katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu, mkoani Lindi juzi. Azam ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# KMKM yaondolewa FA Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAABARIA wa KMKM wameondolewa katika kinyang'anyiro cha mashindano ya kuwania ubingwa wa Kombe la FA Zanzibar baada ya kukubali kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Mafunzo katika mchezo wa hatua ya robo fainali uliochezwa juzi.

Mabao hayo ya Mafunzo katika mechi hiyo yalifungwa na Selemani Idrisa dakika ya 15, Abdulkarim Naim (dakika ya 39), Jaku Joma (dakika ya 56) na Abdulrahman Seif aliyemaliza msumari wa mwisho dakika 89.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema timu yake haikuwa na bahati katika mechi hiyo licha ya kujipanga kufanya vizuri kwenye michuano hiyo.

Msimu alisema baada ya kuondolewa katika michuano hiyo, sasa hivi wataelekeza nguvu kwenye michezo ya Ligi Kuu Zanzibar ambapo watahakikisha wanapambana kusaka ubingwa wa ligi hiyo msimu huu.

"Tumeondolewa katika FA Cup, lakini tunaendelea kujipanga na michezo ya Ligi Kuu Zanzibar ili kuhakikisha tunatwaa ubingwa msimu huu, hatukufurahishwa na matokeo ya FA lakini ndio mchezo," Msimu alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Mafunzo, Abdallah Bakari, alisema baada ya kuingia kwa kishindo hatua ya nusu fainli, timu yake itaendelea kujiimarisha ili kuhakikisha wanacheza fainali ya michuano hiyo. Robo fainali ya pili ya michuano hiyo itachezwa Machi 23, mwaka huu, kwa kuwakutanisha New King dhidi ya Taifa Jang'ombe.

## Dodoma Jiji FC yatangaza hatari

**Na Adam Fungamwango**

ILI kujiweka salama, Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Masoud Djuma amesema timu yake inajipanga imara kuhakikisha haipotezi pointi katika mechi zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo wa zamani wa Simba aliliambia gazeti hili amefanya mazungumzo na wachezaji wake na kuweka mikakati ya ushindi au kutoa sare lakini si kufungwa katika michezo hiyo inayofuata na hatimaye kumaliza msimu kwenye nafasi nzuri.

"Ligi ni ngumu sana na hilo linawafanya hata wachezaji wangu wazidi kupambana. Tumekubaliana kuanzia sasa tusikose pointi yoyote kwenye mechi zilizobaki. Ina maana tunatafuta ushindi ili tuzipate pointi tatu, lakini hata kama tukizikosa tatu, basi tupate hata moja, tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana," alisema Djuma.

Kocha huyo alisema tayari kikosi chake kimekuwa na umoja baada ya kukuta kuna makundi mawili ya wachezaji, hivyo anaamini wataanza kuvuna pointi kutokana na ushirikiano utakaoonyeshwa.

Djuma alijiunga na Dodoma Jiji baada ya kuachana na Mbwana Makata ambaye ndiye aliipandisha timu kutoka Ligi Daraja la Kwanza.

## Serengeti Girls yaenda Botswana

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), iliondoka nchini jana na kuelekea Botswana ikiwa na matumaini makubwa ya kufanya vyema katika mchezo wa marudiano dhidi ya wenyeji utakaochezwa keshokutwa nchini humo.

Botswana itaikaribisha Serengeti Girls katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za U-17 zitakazochezwa baadaye mwaka huu nchini India.

Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime, alisema wanakwenda Botswana kupambana na kamwe hawatabweteka na ushindi walioupata katika mechi ya awali hapa nyumbani.

Shime alisema ari na morali ya wachezaji iko vizuri na matarajio yake ni kupata matokeo mazuri na kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Kila kitu kipo vizuri, wachezaji wana ari na morali ya kufanya vizuri katika mchezo wetu huo wa marudiano dhidi ya Botswana, utakuwa mchezo mgumu na ushindani kwa sababu wenzetu watakuwa nyumbani," alisema Shime.

Serengeti Girls itashuka dimbani keshokuwa ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 7-0 walioupata Machi 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

## ZISIKUPITE

### HAALAND KUTUA CITY

MSHAURI wa Borussia Dortmund, Matthias Sammer amemgusia mshambuliaji wa Norway wa timu hiyo, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21 ataondoka katika klabu hiyo ya Ujerumani na kujiunga na Manchester City. (***Amazon Prime, via Goal***)

### MSHAHARA WA HAALAND

ERLING Haaland anahusishwa pia Real Madrid, lakini anapaswa kupunguza mshahara wake kama atataka kujiunga na vigogo hao wa Hispania. (***Marca***)

### CONTE ANUKIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain imewasiliana na Kocha wa Tottenham, Antonio Conte, ambaye ana kipengele katika mkataba wake wa sasa kinachomruhusu kuondoka Spurs mwishoni mwa msimu. (***Calciomercato, via Football Italia***)

### ARTETA NAYE SOKONI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta yuko katika orodha ya majina ya makocha wanaowaniwa na PSG kumrithi Mauricio Pochettino, lakini Mhispania huyo amesema "ana furaha sana" pale kwa washika bunduki hao wa London. (***Mirror***)

### MESSI HAONDOKI PSG

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi hana mpango wa kutimka PSG, ingawa nyota huyo mwenye miaka 34 amekuwa akihusishwa na klabu yake ya zamani Barcelona. (***Mail***)

### TUCHEL ATAJWA UNITED

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel na bosi wa Sevilla, Julen Lopetegui ni miongoni mwa makocha wanaowaniwa na Manchester United wakati huu klabu hiyo inasaka kocha mpya. (***Guardian***)

### POCHETTINO APINDULIWA

THOMAS Tuchel amempiku Kocha wa PSG, Mauricio Pochettino na kuwa chaguo la kwanza la Manchester United katika nafasi ya kocha mpya wa klabu hiyo ya Old Trafford na ingependa kumteua Mjerumani huyo kabla msimu kumalizika. (***Star***)

### WIJNALDUM KUREJEA EPL

CHAGUO la kiungo wa Timu ya Taifa Uholanzi, Georginio Wijnaldum litakuwa ni kurejea katika Ligi Kuu England kama nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 hayuko kwenye mipango ya muda mrefu ya PSG. (***Teamtalk***)

### LEWANDOWSKI MAMBO BADO

WAKALA wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski amesema hakuna mazungumzo yaliyofanyika kuhusu kuongeza mkataba mpya wa kubakia kwenye klabu hiyo ya Ujerumani. (***Kicker, via 90 Min***)

### ORIGI KUTUA MILAN

KLABU ya AC Milan imeanza mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji mwenye umri wa miaka 26, Divock Origi kwa uhamisho wa bure pale mkataba wake na Liverpool utakapomalizika. (***Calciomercato***)

### LACAZETTE HUYO WEST

KLABU ya West Ham inamtaka mshambuliaji Mfaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 30 ambaye mkataba wake na Arsenal unamalizika mwishoni mwa msimu. (***Teamtalk***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# USHINDI MFULULIZO KICHEKO KWA KLOPP

## Pia kocha huyo afurahia kiwango kilichoonyeshwa na nyota wake huku...

**LONDON,** ENGLAND

JURGEN Klopp amekisifia kikosi chake cha Liverpool baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Arsenal mchezo uliochezwa kwenye dimba la Emirates juzi na kusema ni "maalumu" wakati timu hiyo ikipunguza tofauti ya pointi hadi moja dhidi ya vinara, Manchester City katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Ushindi huo uliamuliwa na mabao ya kipindi cha pili yaliyofungwa na Diogo Jota na Roberto Firmino wakati wekundu hao wakishinda mchezo wao wa tisa mfululizo kwenye ligi hiyo msimu huu.

Arsenal inayonolewa na Kocha Mikel Arteta ilionyesha kiwango cha kuvutia kipindi cha kwanza na walikaribia kupata bao la uongozi kabla ya Jota kufunga la ufunguzi, baada ya shuti la Martin Odegaard kuokolewa na golikipa Alisson.

Akizungumza na Sky Sports baada ya mchezo huo, Klopp alisema ameridhishwa na ushindi wa kuondoka na pointi zote tatu na alikisifia kikosi kwa ushindi huo.

"Kwa hakika ni maalumu," alisema. "Kuja hapa na hali yetu, na hatukuwa na kiwango kizuri kipindi cha kwanza na tukaubadilisha mchezo kuwa wa aina yake.

**"Unatakiwa kuwa kwenye vidole vyao kwa sababu walionyesha tishio kubwa."**

Tangu kuanza kwa mwaka huu, Liverpool imeshinda pointi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu England kuliko timu yoyote), na bado hawajapoteza mchezo wowote wa ligi kwa mwaka 2022.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,042

MECHI KALI
WOLVERHAMPTON
VERSUS
LEEDS
1 | 2.16
X | 3.45
2 | 3.25

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# TUCHEL AWEKA REKODI ULAYA

**PARIS,** Ufaransa

THOMAS Tuchel aliweka rekodi ya ushindi wa mechi nyingi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya mechi 50 kama kocha wakati, Chelsea ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Lille.

Blues hao walipata ushindi pale kwenye dimba la Pierre-Mauroy katika mchezo huo wa pili wa hatua ya 16 uliochezwa juzi na kumfanya Tuchel ashinde mechi 32.

Pia imemfanya kuipiku rekodi ya Zinedine Zidane, ambaye alishinda mechi 31 katika michezo yake 50 za kwanza kwenye ligi hiyo.

Chelsea ilitakiwa kutoka nyuma na kupata ushindi huo wa uwiano wa mabao 4-1 dhidi ya Lille.

Christian Pulisic na Cesar Azpilicueta walipindua meza kwa bao la kwanza la Burak Yilmaz alilofunga kwa penalti.



## Allegri hajutii Juve kutolewa Uefa

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri amesisitiza angecheza kwa staili ile ile licha ya timu yake kutolewa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 na Villarreal hapo juzi.

Bianconeri hao walifungwa mabao matatu ndani ya dakika 12 za mwisho na kikosi hicho cha Kocha Unai Emery, huku mawili yakipatikana kwa penalti, na hivyo kukubali kichapo cha mabao 3-0 pale kwenye dimba la Allianz, kufuatia sare ya 1-1 kwenye mchezo wa kwanza wiki tatu zilizopita.

Kilikuwa kipigo kikubwa zaidi kwa Juve nyumbani katika Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuwafanya watolewe kwenye hatua ya 16 kwa mara ya tatu mfululizo.

Licha ya kichapo hicho, Allegri hajutii namna kikosi chake kilivyocheza na alikataa kuwashutumu wachezaji wake.

"Ningecheza kwa staili ile ile, kwani wachezaji walifanya vizuri kwa dakika 65," alisema akiambia Amazon Prime Italia.

"Kwa wakati fulani, Villarreal walicheza vizuri kwenye safu yao ya ulinzi na tulishinda kuipita.

2,431,860

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/03/22 | 18:00 | Huddersfield vs Bournemouth | 2.51 | 3.29 | 2.65 |
| 02. 19/03/22 | 18:00 | Reading vs Blackburn | 2.60 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 19/03/22 | 18:15 | Eupen vs Mechelen | 2.76 | 3.40 | 2.39 |
| 04. 19/03/22 | 20:45 | GO Ahead Eagles vs Cambuur | 2.48 | 3.45 | 2.70 |
| 05. 19/03/22 | 23:00 | Nantes vs Lille | 2.87 | 2.97 | 2.63 |
| 06. 20/03/22 | 14:30 | Venezia vs Sampdoria | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 07. 20/03/22 | 15:30 | Jahn Regensburg vs Paderborn | 2.75 | 3.24 | 2.45 |
| 08. 20/03/22 | 16:00 | Gaziantep BB vs Galatasaray | 2.71 | 3.36 | 2.45 |
| 09. 20/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Montpellier | 2.40 | 3.45 | 2.80 |
| 10. 20/03/22 | 17:00 | Empoli vs Verona | 3.20 | 3.40 | 2.20 |
| 11. 20/03/22 | 18:00 | Ponferradina vs Eibar | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 12. 20/03/22 | 18:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.41 | 3.34 | 2.89 |
| 13. 20/03/22 | 20:00 | Roma vs Lazio | 2.34 | 3.41 | 2.96 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 18/03/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3303 | MES Rafsanjan vs Zob Ahan | 2.29 | 2.70 | 3.90 |
| 18:20 | 4424 | Al Salmiyah vs AL Tadamon | 1.35 | 4.73 | 6.75 |
| 19:00 | 3139 | Valmiera Fk/Bjss vs Spartaks Jurmala | 1.34 | 4.73 | 6.95 |
| 19:30 | 3934 | NK Radomlje vs ASK Bravo | 2.60 | 3.33 | 2.41 |
| 20:00 | 1750 | Fatih Karagumruk vs Kayserispor | 2.11 | 3.41 | 3.26 |
| 20:00 | 2044 | Backa Topola vs Proleter | 1.40 | 4.26 | 6.58 |
| 20:00 | 2668 | Hrvatski Dragovoljac vs Istra | 3.76 | 3.52 | 1.82 |
| 20:00 | 2739 | Miedz Legnica vs Korona Kielce | 1.75 | 3.42 | 4.23 |
| 20:00 | 2764 | Zaglebie Lubin vs Warta Poznan | 2.20 | 3.07 | 3.12 |
| 20:00 | 5094 | UCD Dublin vs Bohemians FC | 5.22 | 3.82 | 1.55 |
| 20:00 | 5125 | Caykur Rizespor vs Trabzonspor | 4.93 | 3.94 | 1.62 |
| 20:30 | 1186 | Fremad Amager vs Hobro | 2.34 | 3.32 | 2.69 |
| 20:30 | 1336 | SV Horn vs SV Lafnitz | 3.37 | 3.61 | 1.90 |
| 20:30 | 2088 | Austria Lustenau vs Rapid Vienna II | 1.55 | 4.04 | 4.81 |
| 20:30 | 2983 | Austria Vienna II vs SKN St Polten | 2.94 | 3.47 | 2.12 |
| 20:30 | 5057 | Vorwarts Steyr vs Liebherr Gak | 2.45 | 3.42 | 2.50 |
| 20:45 | 5266 | Sassuolo vs Spezia | 1.61 | 4.29 | 4.89 |
| 21:00 | 1474 | Kickers Wurzburg vs Viktoria Koln | 2.65 | 3.29 | 2.51 |
| 21:00 | 5430 | Viseu vs Rio Ave | 4.30 | 3.47 | 1.77 |
| 21:30 | 3633 | Neuchatel Xamax vs FC Winterthur | 3.13 | 3.42 | 2.05 |
| 21:30 | 4912 | CA Fenix vs Defensores Unidos | 3.25 | 2.95 | 2.43 |
| 22:00 | 1317 | Ferencvaros TC vs Mezokovesdi SE | 1.29 | 5.00 | 8.08 |
| 22:00 | 2435 | Heerenveen vs Heracles Almelo | 2.38 | 3.24 | 2.84 |
| 22:00 | 2730 | Telstar vs Dordrecht | 1.82 | 3.86 | 3.62 |
| 22:00 | 4866 | Jong Utrecht vs Jong AZ Alkmaar | 2.22 | 3.47 | 2.89 |
| 22:00 | 4868 | Almere City vs Den Bosch | 1.46 | 4.50 | 5.67 |
| 22:00 | 5652 | Mouscron Peruwelz vs MSK Deinze | 2.69 | 3.32 | 2.43 |
| 22:15 | 3837 | FC Vaduz vs FC Thun | 2.05 | 3.56 | 3.03 |
| 22:25 | 5067 | Amstetten vs Wacker Innsbruck | 2.21 | 3.43 | 2.80 |
| 22:30 | 1479 | Pogon Szczecin vs Wisla Krakow | 1.43 | 4.12 | 6.33 |
| 22:30 | 4510 | VfL Bochum vs Monchengladbach | 2.94 | 3.49 | 2.28 |
| 22:30 | 5241 | Widzew Lodz vs OKS Odra Opole | 1.63 | 3.71 | 4.62 |
| 22:45 | 1957 | Wexford Youths vs Longford Town | 2.89 | 3.32 | 2.21 |
| 22:45 | 2120 | Derry City vs St Patricks | 2.12 | 3.14 | 3.24 |
| 22:45 | 2430 | Shelbourne vs Finn Harps | 2.09 | 3.12 | 3.31 |
| 22:45 | 3286 | Union Saint Gilloise vs Oostende | 1.27 | 5.51 | 9.45 |
| 22:45 | 3526 | Athlone Town vs Galway United | 4.42 | 3.94 | 1.61 |
| 22:45 | 3569 | Carrick Rangers vs Larne | 5.59 | 4.53 | 1.43 |
| 22:45 | 3571 | Newport vs Hartlepool | 1.75 | 3.53 | 4.41 |
| 22:45 | 4817 | Edinburgh City vs Stranraer | 2.40 | 3.34 | 2.61 |
| 22:45 | 5786 | Drogheda Utd vs Dundalk FC | 3.95 | 3.42 | 1.80 |
| 22:45 | 5891 | Dunfermline vs Morton | 2.46 | 3.24 | 2.70 |
| 23:00 | 1112 | Huesca vs Burgos | 1.85 | 3.25 | 4.33 |
| 23:00 | 2257 | Genoa vs Torino | 3.25 | 3.15 | 2.30 |
| 23:00 | 2905 | Wolverhampton vs Leeds | 2.16 | 3.45 | 3.25 |
| 23:00 | 4175 | Athletic Bilbao vs Getafe | 1.73 | 3.39 | 5.39 |
| 23:00 | 5189 | Shamrock Rovers vs Sligo Rovers | 1.49 | 3.93 | 5.76 |
| 23:00 | 5226 | St Etienne vs Troyes | 2.04 | 3.34 | 3.64 |
| 23:15 | 1291 | FC Vizela vs Famalicao | 2.47 | 3.25 | 2.76 |
| 23:30 | 2037 | Univ San Martin vs Carlos Mannucci | 3.26 | 3.31 | 2.03 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# HITIMANA AAHIDI KUVUNJA REKODI YA YANGA LIGI KUU

**Na Dennis Fussi**

KOCHA Mkuu wa KMC, Thiery Hitimana amesema mikakati yao ni kupata ushindi katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopo mbele yao ambao watavaana na Yanga, zote za jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Hitimana amekiri mchezo huo utakuwa mgumu, lakini wapo kwenye uwanja wa mazoezi kuhakikisha wanavuruga rekodi ya Yanga ya kutopoteza mchezo mmoja kwenye ligi msimu huu.

"Tupo kwenye uwanja wa mazoezi tukiweka mipango yetu sawa, lengo ni kuhakikisha tunaifunga Yanga, najua hautokuwa mchezo rahisi kutokana na ubora wao, lakini dhamira yetu ni kuchukua pointi zote tatu kwenye mchezo huo," alisema Hitimana.

Mchezo kati ya Yanga na KMC utachezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Yanga inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 45 baada ya michezo 17 huku KMC ikishika nafasi ya saba kutokana na pointi zake 22.







Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Vijana ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), wakiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere jana kabla ya kuelekea Botswana kuwavaa wenyeji katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za U-17. **PICHA: TFF**



# Kocha Prisons hajakata tamaa

**Na Dennis Fussi**

BAADA ya kupokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Biashara United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Machi 15, mwaka huu, Kocha Mkuu wa Prisons, Patrick Odhiambo amesema bado hajakata tamaa.

Akizungumza na gazeti hili, kocha huyo raia wa Kenya amesema yeye na msaidizi wake, Shabani Kazumba, wamekuwa wakijitahidi ili timu iweze kupata ushindi, lakini bado bahati haijawa upande wao.

"Tunapita katika kipindi kigumu si kwamba tunafungwa eti tunacheza vibaya, tunacheza vizuri isipokuwa makosa madogo ndio yanatuadhibu," amesema Odhiambo.

Maafande hao wa Jeshi la Magereza bado wapo katika nafasi ya mwisho kwenye msimamo wa ligi wakikusanya pointi 13 kwenye mechi 18 za ligi walizocheza.

Michezo
Ijumaa Machi 18, 2022
Nipashe



Allegri hajutii Juve kutolewa Uefa UKURASA 22

KIJAMII ZAIDI...




Wachezaji, viongozi na benchi la ufundi la Yanga wakiwa katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ambapo walikwenda kutoa misaada ya vitu mbalimbali kwa wagonjwa waliolazwa kwenye hospitali hiyo iliyoko jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga yaendelea kuikumbuka jamii

**Na Saada Akida**

BAADA ya jana kuhamasisha wanachama na mashabiki wake kote nchini kujitokeza kuchangia damu, uongozi wa Yanga ulitembelea Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na kutoa misaada ya mahitaji muhimu kwa wagonjwa waliolazwa katika hospitali hiyo.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara wamefanya ziara hiyo ikiwa ni maalumu katika kuadhimisha mwaka mmoja wa kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, marehemu Dk. John Magufuli.

Misaada iliyotolewa ni pamoja na sabuni, maji, mikate, dawa za meno na vitu vingine mbavyo vinavyotumiwa na wagonjwa wa saratani kila siku.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkurugenzi Mwekezaji wa GSM, Hersi Said, alisema Yanga ni ya Wananchi na wao hawakuwa na budi kufanya shughuli zinazohusu jamii.

Hersi alisema hayati Dk. Magufuli alikuwa anagusa maisha ya kila Mtanzania, hivyo waliamua kumwenzi kiongozi huyo kwa namna hiyo, lakini wakimwombea kwa Mungu apumzika kwa amani. Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedrick Kaze alisema vitu walivyotoa msaada vinaweza kuwa ni vichache lakini ni jambo kubwa kwa jamii inayowazunguka.

"Binafsi nawasifu sana viongozi wetu kutoka Yanga na GSM kurudisha fadhila kwa jamii, ni kitu kikubwa tunaomba Mwenyezi Mungu awape nafuu wagonjwa wote," alisema Kaze.

Naye Msemaji wa Yanga, Haji Manara, alisema kilele cha maadhimisho hayo kwa klabu yao kitakuwa kesho kwa kuwataka wanachama na mashabiki wote kufanya usafi katika maeneo ya karibu na matawi yao kwa nchi nzima.

Yanga itashuka dimbani kesho kuvaana na KMC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

# Simba kumaliza makundi kibabe

**Na Saada Akida**

### ●●● Yatamba mikakati ya kuvuna pointi sita imeiva kwa ajili ya kusonga mbele...

UONGOZI wa Simba ya jijini Dar es Salaam umesema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi yao ya Jumapili ili kujiondoa katika hali ya presha wakati kwenye mchezo wao wa mwisho wa hatua ya makundi katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika wanayoshiriki, imefahamika.

**Simba, wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye michuano ya kimataifa itashuka ugenini keshokutwa kuwakabili Asec Mimosas katika mchezo wa tano wa Kundi D.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wamejipanga imara kwa kuweka mikakati mizito ili kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi ya keshokutwa na ya mwisho ya hatua ya makundi na hatimaye kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Ahmed alisema Simba inahitaji kuvuna pointi sita katika michezo hiyo miwili iliyobakia na kumaliza hatua ya makundi wakiwa wanaongoza Kundi D.

"Tumejipanga imara kuhakikisha tunazipata alama sita ikiwamo mchezo wetu wa Jumapili, tutaondoka nchini usiku wa kuamkia kesho (leo), kuelekea Benin kwa ajili ya mechi yetu dhidi ya Asec Mimosas itakayochezwa Jumapili, tunazitaka pointi ili kuziweka vizuri hesabu zetu," alisema Ahmed.

Kiongozi huyo alisema wanafahamu haitakuwa kazi rahisi lakini lengo, matarajio na mipango yetu ni kupata pointi hizo sita, tatu kwa mechi ya Jumapili lakini mchezo mwingine ujao dhidi ya US Gendarmerie.

"Tunakwenda tukijiamini kwa hali ya juu kutokana na ubora wa kikosi chetu, kampeni yetu kwenye mchezo huu tunataka kufuzu ugenini, hilo linawezekana kwa ubora wa kikosi chetu.

"Wana-Simnba wenzangu, mechi ni ngumu lakini kwa maombi yenu pamoja na mapambano tutakayofanya, wachezaji na benchi la ufundi kuendelea kuisuka timu yake, kwa uwezo wa Mungu tutashinda," alisema Ahmed. Aliongeza mipango ya Simba ni kuona wanarejea Tanzania wakiwa wamefikisha alama 10, na ana imani ari ya morali waliyokuwa nayo wachezaji watafikia malengo hayo.

"Wakati mashujaa wetu wakipambana kutafuta pointi tatu huko Benin, mashabiki wa Simba wanatakiwa kuomba dua sana tupate ushindi, lakini kuanza maandalizi ya kuivaaa US Gendarmarie Aprili 3, mwaka huu hapa nyumbani, tunataka kufanya balaa ambalo halijawahi kutokea," alisema meneja huyo.

Naye nahodha msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein, alisema kikosi chao kimejipanga kuweka rekodi mpya msimu huu kwa kupata matokeo mazuri nyumbani na ugenini.

"Tunajua mechi haitakuwa nyepesi, lakini sisi tunakwenda kwenye vita, tumejiandaa kupambana na kamwe hatutawaogopa, watakuwa na presha zaidi kwa sababu tuliwafunga wakiwa ugenini, sasa wao watakuwa nyumbani," alisema beki huyo.

Simba inaongoza Kundi D ikiwa na pointi saba wakifuatiwa na Asec Mimosas wenye alama sita sawa na RS Berkane ya Morocco wakati US Gendarmerie ya Niger yenye pointi nne wakiburuza mkia katika kundi hilo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >